# Nipashe Jumapili

Jumapili Septemba 27, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0580351

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



MAISHA

SEPTEMBA 27, 2020

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili

HARUSI

Ukurasa 12

Ukurasa 10

Usimkatishe tamaa, msaidie aelewe

MAISHA NI NYUMBA

Jiko ni zaidi ya sehemu ya mlo

Ukurasa 15

Chapati za maziwa na siagi

Ukurasa 14

'SIX PACKS'

Mikato yenye maajabu

UKURASA 9



## Lukuvi awashukia wanasiasa madai viongozi kupora ardhi

UKURASA 3

RIPOTI MAALUM

# Hiki hapa chanzo jinsia tata na matatizo yake

**MWANAMKE** aishi kama mwanamume kwa miaka 29, daktari bingwa Muhimbili asema inazuilika iwapo tu...*Endelea Ukurasa wa 4*

## TUNDU LISSU APONGEZA UTENDAJI KAZI WA JESHI LA POLISI

UKURASA 2



Tundu Lissu

IGP Simon Sirro..

## Hasunga awageukia wanaotoza wajawazito

UKURASA 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play

App Store


MICHEZO

YANGA YATAMANI SUKARI YA MTIBWA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# CCM yaahidi umeme visiwani

**Na Mwandishi Wetu, UKEREWE**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeahidi kupeleka umeme kwa wananchi wa Kisiwa cha Gana kilichoko wilayani Ukerewe mkoani Mwanza.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya chama hicho, Kassim Majaliwa, katika mkutano wa kampeni uliofanyika Kitongoji cha Gana.

Mkutano huo ulikuwa mahususi kwa Majaliwa kuwaombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Dk. John Magufuli, mgombea ubunge wa Ukerewe, Joseph Mkundi na madiwani wa wilaya hiyo.

Majaliwa alisema serikali ijayo, kupitia Ilani ya CCM mwaka 2020-2025, itaboresha huduma ya umeme katika visiwa vyote nchini kikiwamo cha Gana chenye wakazi zaidi ya 3,000.

"Mkakati wetu ni kuhakikisha vijiji vyote nchini vinapata umeme, Ukerewe vijiji 70 tayari vina umeme, vimebaki sita ambavyo vitapitiwa na mradi," aliahidi Majaliwa.

Alisema asilimia 80 ya vijiji nchini vimepata umeme baada ya serikali ya awamu ya tano kutekeleza kwa vitendo Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020.

"Serikali itaendelea kuchukua hatua madhubuti kuendeleza na kuimarisha sekta ya nishati ikiwamo kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali. Mpango wa serikali ni kukamilisha usambazaji wa umeme katika vijiji vyote na maeneo ya pembezoni mwa miji," alisema.

Majaliwa alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, serikali imepata mafanikio kwa kuzalisha umeme kutoka megawati 1,308 mwaka 2015 hadi 1,602 mwaka 2020, ongezeko ambalo limeifanya nchi kujitosheleza kwa mahitaji ya nishati hiyo.

Upatikanaji wa umeme kwa jumla Tanzania Bara umeongezeka kutoka asilimia 36 mwaka 2015 hadi asilimia 70. Ujenzi wa miradi umepunguza gharama za kuunganisha umeme vijijini kutoka wastani wa Sh. 454,000 hadi 27,000.

Kuhusu sekta ya uvuvi, Majaliwa alisema serikali imeondoa kodi katika bidhaa mbalimbali za uvuvi ili kutoa fursa kwa wavuvi kujipatia kipato na kuinua uchumi wa taifa.

Alisema tayari serikali imeondoa kodi katika zana na malighafi za uvuvi zikiwamo injini za kupachika, nyuzi za kushonea nyavu na vifungashio.

"Tumedhamiria kuboresha sekta ya uvuvi kwa kuchukua hatua mbalimbali, tumeondoa kodi katika baadhi ya maeneo ili kuhakikisha wavuvi wanapata manufaa kutokana na kazi yao," alisema.

Majaliwa alisema CCM kupitia ilani yake, kitaimarisha ulinzi katika Ziwa Victoria kwa kununua boti za ulinzi ambazo zitawalinda wavuvi wanapokuwa katika shughuli zao za uvuvi.

Alisema kuwa, katika kuhakikisha wavuvi wanafanya kazi kwa ufanisi, serikali iliimarisha ulinzi kwa kuanzisha Kanda Kuu tatu; Ziwa Victoria, Tanganyika na Pwani. Pia zimeanzishwa kanda nne ndogo za Ukerewe, Sengerema, Nyumba ya Mungu na Mtera.

# Lissu alipongeza Jeshi la Polisi

**Na Richard Makore,**
MWANZA

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), amelipongeza Jeshi la Polisi nchini kwa kusimamia haki, sheria na taratibu kipindi hiki cha kampeni za uchaguzi mkuu.

Lissu, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, alimimina pongezi hizo kwa jeshi hilo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema pongezi hizo zimetokana na utendaji wa jeshi hilo, akirejea hali ilivyokuwa katika ziara zake mkoani Geita na Songwe, akikiri kuwa polisi walifanya kazi kubwa ya kuimarisha ulinzi katika mikutano ya kampeni.

Alisema jeshi hilo linafanya kazi kwa weledi, akidai ana ushuhuda wa askari wake kuwadhibiti hata baadhi ya wafuasi wa chama tawala waliotaka kusababisha vurugu kwa kurusha mawe kwenye moja ya mikutano yake.

Katika mkutano wake huo na waandishi wa habari, Lissu pia alitoa ufafanuzi kuhusu CHADEMA kutoweka mabango ya kampeni katika maeneo mbalimbali nchini, akisema limetokana na chama kutokuwa na fedha za kuilipa Mamlaka ya Mapato (TRA).

Lissu ambaye kitaaluma ni mwanasheria, alisema wanaendelea kuomba msaada wa kifedha na watabandika mabango hayo nchi nzima na ikitokea wakazuiwa, watayaweka kinguvu kwa madai kuwa kazi wanayofanya siyo kuzalisha faida.

Mgombea huyo pia alijibu tuhuma za kwamba anatumiwa na mabeberu, akisisitiza kuwa 'ni watu wasiokuwa na akili pekee ndiyo wanachukia mabeberu'.

Lissu alisisitiza kuwa wazungu ambao wanaitwa mabeberu, wakisitisha misaada yao nchini kwa wiki moja, Tanzania haiwezi kuwapo katika kile alichokiita ramani ya dunia.

Katika mkutano wake huo, Lissu pia aliwaahidi Watanzania kuwa, akiingia madarakani kuongoza nchi, atahakikisha anaifuta Idara ya Habari (MAELEZO) ambayo ni chombo cha serikali, akidai haina maana yoyote.

Mgombea huyo alisema mtazamo wake ni kwamba idara hiyo imeanzishwa kwa lengo la kufanya uchunguzi wa habari nzuri ama mbaya zinazoandikwa dhidi ya serikali.

Lissu pia alitumia mkutano huo kunadi sera zake, ikiwamo ya kuwalipa fidia wananchi wote waliobomolewa nyumba zao kupisha miradi ya serikali katika maeneo mbalimbali nchini. Katika mkutano huo, Lissu pia aliulizwa siri ya mikutano yake ya kampeni kuhudhuriwa na idadi kubwa ya wananchi, akijibu kuwa chama chake hakijafanya utafiti kubaini kama wananchi hao wamejiandikisha kupiga kura.

Baada ya mkutano huo, Lissu alikwenda Kisiwa cha Ukerewe kufanya kampeni na leo anatarajiwa kuanza kampeni zake mkoani Mara.



Makamu Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Taifa (Machinga), Steven Susinde (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa tamko la wamachinga wote nchini kumuunga mkono mgombea urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Pombe Magufuli, katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu. Katikati ni Mwenyekiti wa wafanyabiashara wa soko la Magomeni, Nassoro Sakafu na mmoja wa wafanyabiashara wa jiji hilo, Ramadhani Said. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Hasunga awageukia wanaotoza wajawazito

**Na Thobias Mwanakatwe**

TAHARUKI imezuka katika Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe kutokana na kuibuka kwa kikundi kinachojulikana kama Makomandoo ambacho mwanamke sharti ajifungulie kwenye kituo cha afya au zahanati na akibainika amejifungulia nyumbani kwake, anatozwa faini kati ya Sh. 30,000 hadi 50,000.

Kutokana na kikundi hicho ambacho kimeanzishwa kila kijiji na kata, wananchi wamelalamika kunyanyaswa na kudhalilishwa kwa kuwa mwanamke akipata ujauzito, lazima aende akamweleze Komandoo ili awe anafuatilia kama anakwenda kliniki na kama atajifungulia kituo cha afya au zahanati na asipofanya hivyo, faini inamhusu.

Mgombea ubunge wa Vwawa (CCM), Japhet Hasunga, akizungumza na wananchi kwenye mikutano ya kampeni, ametangaza kupiga marufuku kikundi hicho kwa kuwa kinadhalilisha wanawake.

"Kuanzia leo (jana) hakuna cha Komandoo wala nini, tunachotaka mwananchi akiwa mjamzito, aende kliniki kwa wataalamu, unakwenda kumwambia Komandoo una mimba. Je, ana utaalamu kasomea, anajua hata mimba zinakuweje?" Hasunga alihoji huku akishangiliwa.

Hasunga ambaye pia ni Waziri wa Kilimo, alisema kinachosikitisha zaidi ni mama mjamzito hata akienda kliniki anaambiwa ni lazima awe na barua kutoka kwa Komandoo.

"Ni jambo la kushangaza sana kwa mfano mwanamke ana mimba halafu anakwenda kliniki kama kawaida, bahati mbaya uchungu ukamshika, alikuwa yuko shambani kajifungua salama au usiku alikuwa analala uchungu ukamshika kajifungua salama, halafu Komandoo anakuja anasema lazima ulipe faini Sh. 30,000 au 50,000," alisema.

Hasunga alisema mambo hayo hayawezi kukubalika yaendelee katika jimbo hilo na kwamba kuanzia sasa kikundi hicho kiache mara moja kufanya vitendo vya kuwatoza wananchi faini.

Makomando hao waliibuka kufuatia Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kuanzisha mfumo mahususi wa kushirikisha viongozi wa vijiji, kata, madiwani, viongozi wa mitaa na wananchi namna ya kushiriki na kuzingatia elimu ya afya baada ya mama kubainika kuwa na ujauzito.

Mratibu wa Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto Wilaya ya Mbozi, Alexia Nonjela, alisema kutokana na tatizo la vifo vya watoto wachanga na watoto chini ya miaka mitano ambavyo vimekuwa vikiripotiwa mara kwa mara na vyombo vya habari pamoja na idara ya afya, waliamua kuanzisha utaratibu uitwao UTURO wakilenga kukomesha kabisa vifo hivyo.

Alisema UTURO ni mfumo uliouchukua katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbalali mkoani Mbeya ambako kwa kiasi kikubwa halmashauri hiyo walifanikiwa kushirikisha jamii katika kuhakikisha wajawazito wote chini ya miezi mitatu kuanza kuhudhuria kliniki na kukomesha kabisa vifo vya mama na mtoto.

Nnonjela alisema mkakati huo unashirikisha viongozi wa mitaa, vijiji, madiwani na wananchi ambapo kwa pamoja wanachagua wanawake watatu, maarufu makomando wanaojua kusoma na kuandika na wenye sifa za kujitolea, kuwa na siri, upendo na waaminifu ambao hutoa elimu na taarifa zote za kinamama wanaopata ujauzito kuhakikisha wanahudhuria kliniki baada ya miezi mitatu ya mwanzo.

HABARI KITAIFA

# Bajeti ya Bunge Afrika Mashariki Dola milioni 97.6

**Na Asraj Mvungi,** ARUSHA

BAADA ya mvutano wa muda mrefu kuhusu maslahi ya Wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA), hatimaye Bunge hilo limewasilisha makadirio ya bajeti yake ya mwaka wa fedha 2020/21 ya Dola za kimarekani milioni 97.6

Bajeti hiyo imewasilishwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya hiyo, Prof. Nshuti Manase, ambaye pia ni Waziri anayeshughulikia Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Mambo ya Nje wa Rwanda.

Akiwasilisha makadirio ya bajeti hiyo kwenye kikao hicho kilichofanyika kwa njia ya mtandao, Prof. Manase, alianisha kuwa katika bajeti hiyo ambayo imepungua kutoka Dola milioni 116.4, kipaumbele kikubwa kimeelekezwa kwa sekretarieti ya jumuiya hiyo iliyotengewa Dola milioni 48.56 huku Bunge likitengewa dola milioni 16.75

Maeneo mengine yaliyopewa kipaumbele ni pamoja na baraza la vyuo vikuu ambalo limetengewa dola milioni 10.97, Kamisheni ya Ziwa Victoria (dola milioni 8.38), Mahakama ya Afrika Mashariki (Dola milioni 3.97) na Kamisheni ya Kuendeleza Uvuvi katika Ziwa Victoria Dola milioni 3.07.

Pia bajeti hiyo inaonyesha kuwa Kamisheni ya Sayansi ya Teknolojia imetengewa Dola milioni 1.53, Kamisheni ya Kiswahili Dola milioni 1.38 na mamlaka ya Ushindani Afrika Mashariki dola milioni 1,12. Katika kufanikisha bajeti hiyo, kila nchi itatakiwa kuchangia dola.

Kulingana na bajeti hiyo, mwaka huu nchi wanachama zitatakiwa kuchangia asilimia 57 ya bajeti na kiasi kilichobaki kitatolewa na wahisani na kwa mujibu wa mwenyekiti huyo. Wabunge wanaratajia kuanza kuijadili bajeti hiyo wiki ijayo.

# Lukuvi awashukia wanasiasa madai viongozi kupora ardhi

**Na Waandishi Wetu,** IRINGA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi amekanusha vikali kauli iliyotolewa na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa kuwa kuna baadhi ya viongozi wamepora ardhi katika maeneo mbalimbali ikiwamo Mbarali mkoa wa Mbeya.

Mbali na kukanusha, Waziri Lukuvi amesisitiza kuwa kati ya viongozi waliotuhumiwa kuhusika na suala hilo, hakuna hata kiongozi mmoja aliyefanya hivyo.

Licha ya kuweka msimamo huo wa serikali, Waziri Lukuvi amesisitiza kuwa umilikishaji ardhi nchini unafuata sheria na serikali haina ubaguzi katika kutekeleza hilo kwa mtu yeyoye. Pia amesema umilikishaji ardhi kwa mtu yeyote hauna kikomo.

Lukuvi asema hayo jana mjini hapa alipokutana na waandishi wa habari kufafanuzi wa baadhi ya kauli zilizokuwa zikitolewa na viongozi wa vyama vya siasa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

"Serikali haina ubaguzi wa kumilikisha ardhi na mwananchi yeyote bila kujali itikadi ya chama cha siasa anaweza kumilikishwa" alifafanua Lukuvi.

Kwa mujibu wa Lukuvi, serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kushughulikia masuala ya ardhi likiwamo la kuvibakisha vijiji 920 kati ya 975 vilivyokuwa kwenye hifadhi na kubainisha kuwa serikali inaangalia namna ya kuvibakisha vijiji vingine 55 vilivyosalia.

Kuhusu suala la Mbarali, alisema wananchi wanaoishi katika vijiji 29 eneo la Mbarali wameamuriwa kubaki eneo hilo ingawa kwa mujibu wa Gezeti la Serikali (GN) Namba 28 la mwaka 2008, walitakiwa kuondoka lakini kwa huruma, Rais John Magufuli alibatilisha uamuzi huo na kuagiza vijiji visiondolewe.

"Wananchi wa Mbarali waendelee kuishi kama wanavyoendelea. Mgogoro wa Mbarali ni wa muda mrefu tangu mwaka 2008 na serikali ya awamu ya tano haipaswi kulaumiwa na Rais Magufuli si mtu wa kubeza kwa kuwa vijiji vilitakiwa kuondolewa lakini aliamuru vibaki," alisema.

Waziri huyo alisema baada ya uamuzi wa kutoviondoa vijiji 920 kati ya 975, hatua inayofuata ni kupima upya mipaka sambamba na kupanga mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kubainisha matumizi ya maeneo husika.

Lukuvi pia alisema serikali katika kuwajali wananchi, imeamua pia kufuta mapori tengefu 12 yenye zaidi ya hekta 707,659.4 sambamba na kumega hifadhi 14 za misitu kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji.

Aliongeza kuwa, serikali ya awamu ya tano imeendelea kuchukua hatua za kupunguza na kufuta mashamba makubwa kwa wamiliki waliokiuka masharti ya umiliki na kubainisha kuwa kwa sasa serikali imeshafuta mashamba yasiyopungua 49 na kugawiwa kwa wananchi.

Kuhusu tatizo la ardhi katika mkoa wa Morogoro, Waziri Lukuvi alisema kazi ya uhakiki mashamba 11 katika wilaya ya Kilosa imekamilika na muda ukiruhusu watatangaziwa mashamba yaliyofutwa kutokana na wamiliki wake kukiuka masharti ya umiliki.

Katika hatua nyingine, Waziri Lukuvi waliwaonya wananchi wote waliomilikishwa ardhi kuhakikisha wanafuata sheria na kusisitiza kuwa sheria za ardhi zimewekwa ili kutekelezwa na wasiozifuta watafutiwa umiliki na kupatiwa watu wengine.

**■Imeandikwa na FRANCIS GODWIN na MUNIR SHEMWETA.**



Mgombea Ubunge wa Jimbo la Muhambwe, wilayani Kibondo, mkoani Kigoma kwa tiketi ya chama cha ACT Wazalendo, Julius Masabo akiwaomba kura wakazi wa Kibondo mjini, wakati wa mkutano wa uzinduzi wa kampeni za mgombea huyo, juzi. **PICHA: SAID POWA**

# Abbasi: SGR itachochea kasi ya maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

UJENZI wa Reli ya Kisasa (SGR) umeelezwa kuwa utachochea maendeleo ya watu kwa kurahisisha muda wa usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo kwa mwendokasi.

Hatua hiyo itapunguza muda mwingi unaopotea barabarani na kuwafanya wananchi kuwahi kufanya kazi zingine za maendeleo.

Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbasi, amesema hayo jana Ihumwa jijini Dodoma wakati anawaaga viongozi wa wizara hiyo kuanza ziara ya kutembelea mradi wa SGR ili kujionea maendeleo yake. "Wizara ya Habari ni wizara muhimu sana katika nchi yetu na mradi huu pia. Ndiyo wizara yenye dhamana na habari kwa maana hiyo tumekuwa tukiutangaza sana na kuulinda mradi huu ili kuwaonyesha Watanzania nini kinaendelea kwenye huu mradi," alisema.

Dk. Abbasi amesema Tanzania iko makini kuwekeza kwenye mambo ambayo ni muhimu katika kuleta manufaa na maendeleo ya watu na kusisitiza kuwa ni utamaduni mpya kuwa na taifa la wachapakazi, kuwa Watanzania wanaojiamini na kuwa watu wanaopenda mambo mazuri ambayo yanaletwa na serikali kwa manufaa ya wananchi wake.

"Tunaposema huu ujenzi wa reli ni kitu, ndiyo ni kitu. Reli ya SGR ni kitu kinachokwenda kuleta maendeleo ya watu. Utakapoweza kusafiri kwa muda mfupi kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, umepunguza muda mwingi wa kupoteza barabarani na kuwahi kwenda kufanya kazi,"alisisitiza. Huu ni moja miradi mikubwa inayotekelezwa na serikali nchini na kuwa miongoni mwa miradi mikubwa Afrika. Serikali imewekeza trakriban Sh. trilioni saba kwa kipande cha Dar es Salaam, Morogoro hadi Mkutupora ambapo kipande cha Morogoro hadi Dodoma kimefikia asilimia 42 hadi kukamilika kwake.

Meneja wa Mradi Kipande cha Morogoro hadi Mkakutupora, Mhandisi Mteshi Tito, alisema reli hiyo itatumiwa na treni ya abiria ambayo itakuwa na mwendo wa kasi ya kilometa 160 kwa saa na ya mizigo itatumia saa moja kwa kilometa 120 hatua inayofanya mradi huo kuwekewa uzio kuanzia mwanzo hadi mwisho ili kuepusha mwingiliano wa watu.

Mhandisi Tito aliongeza kuwa kipande cha reli ya SGR kati ya Morogoro na Mkutupora, kina kilometa 422. Kilometa 336 zinajumuisha njia kuu na 86 sehemu za kupishania treni.

MAKALA MAALUM



# Hiki hapa chanzo jinsi tata na matatizo yake

## ■Mwanamke aishi na jinsi ya kiume kwa miaka 29
## ■Mtaalamu Muhimbili asema inazuilika iwapo tu...

**Na Mary Geofrey**

JINSI tata ni mtoto kuzaliwa akiwa hana baadhi ya viungo vya mwanamke au mwanamume na hivyo kushindwa kutambulika kama ni wa kike au kiume.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Watoto katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Zaituni Bohari (pichani), anaeleza kwa kina kuhusu tatizo hili kuanzia visababisho vyake, namna linavyotibiwa na njia za kuepuka kupata watoto wenye jinsi tata.

Anasema mtoto mwenye jinsi tata, anaweza kuzaliwa akiwa na sehemu yake ya jinsi ya kike ikiwa na upungufu wa kimaumbile na vilevile kuwa na maumbile ya siri ya kiume ambayo hayajajitosheleza kwa kiasi kikubwa ikiwamo ukosefu wa korodani.

"Hali hii huwafanya wazazi wanapozaa watoto wa aina hii kuamua kuwapa jina kulingana na na walivyomuona na kumhisia atakuwa wa jinsia gani," anasema Dk. Bohari.

Mtaalamu huyo wa afya anasema hatua ya kwanza ya kubaini tatizo hilo inapaswa kuanzia kwa mkunga anayemzalisha mama, akisisitiza kuwa anapaswa amkague mtoto kila eneo la mwili kabla ya kumkabidhi kwa mama yake.

Dk. Bohari anasema katika maeneo ya vijijini ambako kuna uhaba wa watumishi wa afya, wakunga hukagua baadhi ya vitu kama uzito wa mtoto, jinsia yake, kama mtoto amelia au hajalia na kumkabidhi mama.

Anasema katika baadhi ya hospitali nchini, wataalamu wa afya hawana uelewa wa kuwakagua kwa kina watoto kabla ya kuwakabidhi kwa mama zao, akisisitiza ndiyo sababu wazazi wengi hubaini tatizo hilo wakiwa nyumbani wakati wa kumwogesha au kumvalisha nguo.

Anasema baada ya mama kubaini tatizo hilo, baadhi huamua kwenda kituo cha afya kutoa taarifa ili mtoto afanyiwe uchunguzi wa kina na wengine hukaa kimya.

"Nitumie fursa hii kutoa wito kwa wazazi, ukiona mtoto amezaliwa akiwa mwenye jinsi tata, tafadhali usikae kimya, wahi kutoa taarifa katika kituo cha afya kilicho karibu ili aanze kupatiwa matibabu," anaonya Dk. Bohari.

**MATIBABU MUHIMBILI**

Dk. Bohari anasema kwa sasa Muhimbili wanapokea wagonjwa wengi wenye jinsi tata wakitoka maeneo mbalimbali nchini na wamekuwa wakipatiwa matibabu katika kitengo chao cha watoto wadogo.

Anasema watoto wachache wanafikishwa hospitalini huko wakiwa na umri wa chini ya miezi sita na wengi wao wanaofikishwa kwao ni wenye umri wa kuanzia miaka miwili.

"Tunapokea wa miezi mitatu, miezi sita ila wengi ni wa umri wa kuanzia miaka miwili hadi sita na tulishapokea hadi mgonjwa mwenye umri wa miaka 29," anasema Dk. Bohari.

Anasema kijana huyo (29), alilelewa kama mtoto wa kiume kwa miaka yote, lakini alipofikishwa Muhimbili walibaini kuwa alikuwa na jinsi ya kike.

"Tulipomfanyia uchunguzi wa kina, ndipo tukagundua huyu wa kike. Changamoto kubwa inayokuja ni huyu ameshaishi maisha kama mtoto wa kiume, amefanya kazi na kiume na ameshajizoesha kuwa yeye ni wa kiume, leo umwambie yeye ni mwanamke, unaweza kuona kama unaweza kuvaa viatu vyake," anasema.

Dk. Bohari anaeleza kuwa, baada ya kuwafikisha hospitalini hapo, watoto huanza kuwafanyia uchunguzi wa kina, kuangalia vipimo vya kawaida vya damu, wingi na seli za damu kama zipo kawaida, wanakwangua seli kwenye midomo ambazo zikichunguzwa zinaonyesha jinsi ya mtoto, kama ni wa kiume au wa kike.

Anasema pia wanaangalia vichocheo vya mwili na kujua homoni zake kama ni za kike au za kiume na vipimo vingine vya kina.

Anasema wanafanya uchunguzi kwa kumpeleka mgonjwa chumba cha upasuaji kwa ajili ya kipimo cha viwango vya 'dhahabu' ambao ni utaalamu wa uchunguzi wa njia ya matundu madogo madogo ya mwili kwa kutumia kompyuta.

Dk. Bohari anasema chumba hicho kinakuwa na wataalamu wa kutosha ili kuthibitisha uhalisia wa jinsi yake kwa sababu huonyesha via vya uzazi vya mwanamke au mwanaume kwa uhalisia.

"Kipimo hiki tunakiita Gold Standard ambacho hakiyumbishi majibu ya kufahamu jinsi halisi ya mtoto," anaeleza Dk. Bohari.

Anasema pia wanachukua kipimo cha vinasaba vya binadamu (DNA) ili kuendelea kukusanya ushahidi wa majibu halisi ya jinsi ya mtoto. Dk. Bohari anasema, baada ya majibu yote hayo, wanakutana jopo la madaktari wa watoto, usingizi, saikolojia, uzazi, bingwa wa kinamama, mwanasheria wa hospitali na bingwa wa akili.

"Wote mnakaa kamati ya kujadili majibu ya vipimo vyote na kutoa uamuzi wa pamoja wa kufanya upasuaji wa kumweka mtoto kwenye jinsi yake anayostahili.

"Katika hili, wazazi ndiyo wanaamua kuhusu aina gani ya jinsi apewe mtoto wao, lakini kwa wenye umri wa zaidi ya miaka 18, wanatakiwa kuamua wenyewe," anasema Dk. Bohari.

Anasema baada ya kujiridhisha, ndipo wanafanya uamuzi wa kufanyia upasuaji kwa ajili ya kupangilia jinsi halisi ya mtoto.

Anasema pia wanatoa dawa kwa ajili ya kuongeza homoni za kike au kiume na kufanya upasuaji wa kurekebisha maumbile ya kike au ya kiume.

Daktari huyo anasema kuwa, baada ya kumaliza kufanya upasuaji, wanashauri familia kuhama eneo walilokuwa wakiishi awali, mtoto kuhamishwa shule (kwa aliyekuwa ameanza shule) na pia wanafanya kliniki ya kuonana na madaktari bingwa wa saikolojia.

Mtaalamu huyo anabainisha kuwa, tayari hospitali hiyo imefanya upasuaji wa kubadilisha maumbile kwa watu sita tangu ianze kutoa matibabu hayo ya kibingwa.

"Kuna mtoto wa kike ambaye alikuwa akiishi maisha kama wa kike, alishatobolewa hadi masikio, lakini tulimbadilisha kuwa wa kiume na sasa yuko darasa la tatu na anaendelea vizuri na maisha kama mtoto wa kiume," anasema Dk. Bohari.

"Niiombe jamii itambue wazi kuwa huu nao ni ugonjwa kama yalivyo magonjwa mengine, wazazi wanatakiwa kuwapeleka hospitali watoto wao ili wafanyiwe vipimo na wanapobainika kuwa na jinsi tofauti, afanyiwe upasuaji wa kumrekebisha," anashauri.

Dk. Bohari anafichua kuwapo kwa tatizo la wazazi kuficha watoto wao wakifikiria mtazamo wa jamii kama itawatenga na hata kuwaona wakosaji.

Anasema kutojitokeza kwenda hospitalini nalo ni tatizo linalowaumiza watoto kwa sababu kuna wengine wanaishi kama wanaume, lakini wanapata hedhi, hivyo hali hiyo inawatesa zaidi.

Anasisitiza kuwa matibabu wanayotoa ni ya siri kati ya daktari na mgonjwa, hivyo wazazi wanapaswa kujitokeza ili kuwatibu watoto wao.

**KIINI CHA JINSI TATA**

Mtalaamu huyo wa matibabu ya watoto anasema tatizo hilo linatokana na vichochezi vya mwili na kwa baadhi ya watu linachangiwa na kurithi.

Daktari huyo anasema hakuna sababu ya msingi kwa mtoto kuzaliwa na jinsi tata, lakini kuna viashiria vya sababu za kutokea kwa shida hiyo ya kimaumbile.

Anasema viashiria hivyo ni mama akiwa mjamzito kutotumia madini chumvi ambayo yana kazi ya kujenga msingi imara wa mtoto kuzaliwa bila kasoro yoyote.

Anasema mama akihudhuria kliniki na akapewa madini chumvi ambayo yanalinda mtoto azaliwe akiwa salama hasa katika kipindi cha miezi mitatu ya mwanzo, ni vigumu kupata mtoto mwenye tatizo hilo.

Anasema mama akiwa kliniki, anapewa ratiba ya kula vyakula vyenye virutubisho kwa mpangilio bora.

"Wito wangu kwa mama wajawazito na wanaotarajiwa kubeba ujauzito, wajitokeze kupata ushauri wa kina ambao wanapewa kusaidia mtoto kuzaliwa bila kasoro," anashauri.

Dk. Bohari anasema, mama mjamzito pia anapaswa kula vyakula vyenye protini na mboga za majani kwa wingi na kutumia mafuta ya mimea.

Anabainisha kuwa vikwazo vingi vinavyojitokeza kwenye uzazi vinatokana na maisha watu wanayoishi ya kula vyakula visivyomjenga mtoto.

Dk. Bohari anawatoa hofu Watanzania kuwa gharama za matibabu hayo ni kama za magonjwa mengine na kuna unafuu kwa watoto ambao watakuwa wanatumia bima ya afya.

MAKALA MAALUM -2

# Hii ndiyo hatari kuu ya ndoa za ‘kaka na dada’

## ■TEC, BAKWATA wapaza sauti
## ■Wanasheria waonya maharimu



Na Romana Mallya

SEHEMU ya kwanza ya makala haya Jumapili iliyopita, ilianika madhila na hatari ya ndoa za kaka na dada, picha kuu ya matatizo yanayofungamana na uhusiano wa aina hiyo, huku wadau wa kijamii na kitabibu wakiwasilisha ushuhuda wa namna wahusika wanavyoingia kwenye matatizo kijamii na kiafya.

Katika hilo, Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) lina maoni yake. Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Baraza hilo, Padri Chesco Msaga, anasema wao wanakitafsiri kama kitendo haramu kwa sababu kinakinzana na maandiko ya kiimani wanayoyasimamia, ambayo kimsingi ni rasmi kitaifa na kimataifa. Vivyo hivyo, msemaji huyo wa asasi hiyo yenye ufuasi mkubwa kitaifa, anaitaja kadhia hiyo kuwa kijamii nako iko nje ya mipaka ya uhalali, binafsi akiibatiza ‘ndoa haramu’.

Anaendelea: “Kanisa tunakemea sana hili, sheria za kanisa zinaelekeza watu wenye uhusiano wowote wa damu, iwe watoto wa mjomba, baba mdogo au wakubwa na undugu mwingine, hawawezi kuoana.”

Hata hivyo, anasema matukio ya aina hiyo ni nadra kutokea kanisani kwa kuwa wana utaratibu unaowataka wahusika kabla ya kufunga ndoa, lazima wapeleke vyeti vya ubatizo kanisani.

“Ni mara chache inaweza kutokea, maana lazima wahusika waeleze asili zao ni zipi. Tatizo linakuja pale wamefunga ndoa ya mila baadaye wanakuja kanisani ili kuibariki, ukiwauliza ndipo wanabaini ni ndugu,” alisema.

> **“Ni mara chache inaweza kutokea, maana lazima wahusika waeleze asili zao ni zipi. Tatizo linakuja pale wamefunga ndoa ya mila baadaye wanakuja kanisani ili kuibariki, ukiwauliza ndipo wanabaini ni ndugu.”**

Kiongozi mwingine wa kidini, Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum, anasema inapotokea ndugu kuoana ni laana na haliruhusiwi na ikitokea jamii ikaenenda katika hilo, itapata janga la maradhi.

“Mwanadamu ametofautishwa na wanyama ndiyo maana tuna shangazi, mama mdogo, kaka, dada na wengine wengi, kitu ambacho kwa wanyama hakuna. Wanaofanya hivyo (ndugu wanaooana), wanajitoa kwenye utu, kinakuwa ni kizazi chenye laana kubwa,” anasema.



Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum

**WANASHERIA**

Nipashe ilidai ufafanuzi wa kisheria kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, ambaye anasema ipo sheria inayokataza ndugu kuoana.

Henga anarejea Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, ambayo inawakataza ndugu kuoana ikiwapa tafsiri ya kitaalamu kwamba ni ‘maharimu’.

Kwa mujibu wa tafsiri rasmi ya lugha kutoka kwenye Kamusi ya Kiswahili Sanifu, maharimu ni mtu ambaye huwezi kumuoa au kuolewa na naye kwa sababu ya unasaba.

“Wale wanaoamua kufunga ndoa wasiwe na uhusiano wa karibu kindugu. Inakatazwa katika kifungu cha 14 cha Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 mtu kuoa au kuolewa na mzazi wake, mtoto au mjukuu wake, kama ni dada yake, mama au shangazi au baba wa mjomba wake, baba au mama wa kambo na mwanaye aliyemfanya kuwa mtoto wake,” alisema.

Henga anabainisha uamuzi wa kisheria katika matukio ya aina hiyo, akifafanua kwamba sheria hiyo haina adhabu, bali inabatilisha uhalali wa ndoa ya aina hiyo.

Ofisa Habari wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita), Hadija Mzava, anasema kuwa mchakato wa ubatilishaji ndoa unaanzia mahakamani na ndiko uhalali wa mabadiliko kisheria hupatikana.

Anasema wahusika wakishafika mahakamani, huwa hawapeani talaka kwa kuwa ndugu kuoana ni ndoa batili na haina talaka.

“Inapotokea kesi ya aina hii ikienda mahakamani, mahakama itatoa uamuzi wote, baadaye wataleta RITA uamuzi uliobatilisha, na ndoa hizi hazina talaka,” anabainisha.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kwa pongezi hizi Polisi waongeze weledi katika wa utekelezaji majukumu

**MGOMBEA** Uraia kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, jana alizungumza nabo vya habari jijini Mwanza ikiwa ni sehemu yake ya kampeni za kuwania nafasi hiyo, zinazoendelea kwa kufanya mikutano ya ndani nay a nje sehemu mbalimbali nchini.

Pamoja na mambo mengine, Lissu alilipongeza Jeshi la Polisi nchini kwa kutekeleza wajibu wake ikiwamo kusimamia amani na utulivu, haki, sheria na taratibu katika mikutano hiyo ya kampeni za uchaguzi zinazoendelea kwa ujumla.

Lissu alitolea mfano wa mikutano yake katika mikoa ya Songwe na Geita kuwa polisi walifanya kazi nzuri katika kulinda na kuweka mipaka ya mgombe kutokufikiwa na watu wenye nia ovu.

Mgombea huyo hakuishia hapo tu kwani alisema polisi hao walifikia hatua ya kurusha mabomu dhidi ya watu aliowaita wafuasi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) waliokuwa wakijaribu kufanya vurugu ikiwamio kurusha mawe kwenye mikutano.

Kutokana na kauli hiyo, ni dhahiri kwamba Jeshi la Polisi limetekeleza wajibu wake ambao pamoja na mambo mengine, ni kulinda usalama wa raia na mali zao wakati wote. Katika mikutano ya kampeni kuelekea uchaguzi, polisi wamepewa jukumu la kulinda usalama kwenye mikutano ili kuhakikisha kampeni zinafanyika katikia hali ya amani na utulivu.

Sifa hizo kwa Jeshi la Polisi zimekuja wakati ambao kumekuwa na malalamiko dhidi ya chombo hicho kwamba kimekuwa hakitendi haki kwa vyama vya upinzani kwa kuwa askari wake wamekuwa wakiwanyanyasa hata kuwatawanya wapigakura wanaohudhuria mikutano hiyo.

Itakumbukwa kwamba katika mikutano au matukio mengi ya vyama vya upinzani, kumekuwa na taarifa kwamba polisi wamekuwa wakitumia nguvu kupita kiasi kuwadhibiti wanasiasa wa upinzani na wafuasi wao.

Wakati mwingine, imekuwa ikidaiwa kuwa polisi wanatumia mabavu na hata kussababisha uvunjifu wa amani. Moja ya mifano ni tukio la Kinondoni wakati wa uchaguzi mdogo wa ubunge katika jimbo hilo ambapo polisi walipambana na wafuasi wa CHADEMA na hata kusababisha mauaji ya raia aliyekuwa kituo cha basi.


Kutokana na tukio hilo, kwenye moja ya mikutano ya makamanda na maofisa wakuu wa polisi, Mkuu wa Jeshi hilo, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, alisema polisi wanapaswa kujitafakari na kutotumia nguvu za ziada katika kutekeleza majukumu yao, huku akitolea mfano wa tukio la Kinondoni kwamba kama busara ingetumika huenda maafa kama yale yasingetokea.

Pongezi zilizotolewa na Lissu ni ishara kwamba askari wamezingatia maagizo ya mkuu wao juu ya kufanya kazi kwa weledi pamoja na kutokuwa na ushabiki wa upande wowote katika kutekeleza kazi zao za kila siku, ikiwamo katika kipindi hiki cha kampeni kuelekea uchaguzi mkuu.

Kwa upande mwingine, hatua ya upinzani kulipongeza Jeshi la Polisi ni kitu kigeni katika siasa za Tanzania kutokana na ukweli kwamba, upande huo wa kisiasa umekuwa ukidai mara kwa mara kwamba hauna imani na chombo hicho. Hiyo ni hatua mpya na inaonyesha ukomavu wa kisiasa. Pamoja na hayo, pongezi hizo ziwe chachu kwa polisi kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi.

Pamoja na hayo, ni vyema kwa Watanzania kujenga utamaduni wa kupongeza mambo mazuri yanayotendekea katika upande mwingine bila kujali imani wala itikadi ya kisiasa. Kuwapo kwa upinzani hakumaanishi ni kukosoa kila jambo bali kinachotakiwa ni kubeza au kuponda kile kinachofanywa vibaya na kupongeza kila kizuri kinachofanywa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Madereva wa barabara hii mwendo wenu haufai

**KABLA** ya mwaka 2017, barabara ya kutoka Mbezi Mwisho kwenda Kinyerezi, jijini Dar es Salaam, ilikuwa kero kwa madereva wa vyombo vya moto na hata kwa abiria.

Kero hiyo ilitokana na ubovu wa barabara hiyo kwa kuwa haikuwa na lami, hivyo wakati wa mvua ilikuwa haipitiki kirahisi kwa sababu ya kujaa tope lililosababisha magari kunasa.

Si tope tu bali wakati mwingine maji ya mvua yalijaa barabarani na kukata mawasiliano kati ya Mbezi na Kinyerezi. Lakini pia wakati wa kiangazi ilikuwa kero kutokana na vumbi kutimka na kusababisha watu kupata mafua.

Lakini pia si kwamba magari ya abiria yalikuwa mengi, la hasha, yalikuwa machache. Madereva wengi walikuwa wakiikwepa kutokana na kero hizo, na wale waliokuwapo walikuwa wakitoza nauli ya Sh. 1,000 kwa kila abiria.

Bahati nzuri ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami na yenye urefu wa kilometa nane ulikamilika mwaka 2017 na tayari kuna ruti za daladala kutoka Mbezi Mwisho, kuelekea Gongo la Mboto, Tandika na Segerea.

Hatua hiyo imesaidia kuwaondolea abiria kero ya kuzunguka Ubungo kwenda katika maeneo hayo, badala yake wanapitia Msigani, Malamba Mawili, Kifuru, Kinyerezi hadi kufika kule wanakokwenda.

Barabara hiyo imesaidia kurahisisha usafiri, lakini bahati kuna tatizo ambalo ni vyema nikaliweka wazi ili wahusika wajirekebishe kabla halijasababisha madhara kwa abiria na hata waenda kwa miguu.

Tatizo ni uendeshaji kasi wa madereva wa magari na bodaboda unaofanywa na madereva wasiozingatia sheria za usalama barabarani. Hali hii kama haitadhibitiwa, inaweza kusababisha ajali ambao wakati mwingine zingeweza kuzuilika.

Kwa wasioifahamu barabara hiyo ni kwamba ina miinuko na kona nyingi, hivyo suala madereva kuchukua tahadhari ikiwamo kutoendesha kwa mwendo uliopitiliza ni la muhimu.

Si kuzingatia kuendesha kwa tahadhari tu, bali pia kutosimama kwenye kona na kubeba abiria, kwa kuwa kufanya hivyo bado kunaweza kusababisha ajali ambazo zinatokana na uzembe.

Ninauita uzembe kwa sababu dereva

> **Tatizo ni uendeshaji kasi wa madereva wa magari na bodaboda unaofanywa na madereva wasiozingatia sheria za usalama barabarani. Hali hii kama haitadhibitiwa, inaweza kusababisha ajali ambao wakati mwingine zingeweza kuzuilika.**

anayejua kazi yake hawezi kukubali kusimamisha gari kwenye kona na kupakia abiria, kwa kuwa kufanya hivyo ni kutafuta ajali zisizo za lazima.

Madereva wasisubiri ajali zitokee ndipo wachukue hatua, bali ni vyema wakatambua kuwa kinga ni bora kuliko tiba ingawa ni kweli ajali haina kinga, lakini umakini unahitajika wawapo barabarani.

Moja ya sababu ambazo huwa zinatajwa kuchangia ajali za barabarani ni makosa ya kibinadamu, ikiwamo uzembe wa madereva ulevi, mwendokasi na ubovu wa vyombo vya moto na mchango wake unaelezwa kuwa ni asilimia 70.

Sababu hizo zote ziko ndani ya uwezo wa madereva, hivyo jambo la msingi ni wao kuendesha vyombo hivyo huku wakizingati sheria za usalama barabarani ili kuepuka ajali ambazo zinaweza kusababishwa na sababu hizo.

Kama nilivyoeleza awali, barabara ya Mbezi Mwisho kupitia Malamba Mawili hadi Kinyerezi, ina miinuka na kona nyingi, ambazo ni muhimu dereva kuwa makini kwa kuepuka kuendesha mwendo usiyofaa.

Vilevile anatakiwa kuepuka kusimama kwenye kona kupakia abiria kama njia mojawapo ya kumhakikishia usalama na abiria wake, kuliko kufanya uzembe ambao matokeo yake ni kuisababisha ajali.

Nimegusa sana madereva wa magari ya abiria kwa sababu wengi wao ndio wanaofanya uzembe huo wa kuendesha magari kwa mwendo usiofaa na hata wakati mwingine kusimama kwenye kona na kupakia abiria. Hali kama hiyo si salama kwao na kwa abiria pia, wasisubri wapate ajali ndipo wachukue hatua, badala yake wanatakiwa kuwa makini wakati wote wawapo barabarani ili kuepusha ajali.

Bila madereva kuchukua hatua mapema, huenda zikatokea ajali na kusababisha watu kupoteza maisha au kuwa na ulemavu wa kudumu ambao wakati mwingine humfanya mtu kushindwa kufanya shughuli zake za kila siku.

Kabla ajali hazijatokea, ni vyema wahusika wakachukua hatua za kuwa makini mapema kwa ajili ya usalama wao na wa abiria pia, kwani kupunguza ajali inawezekana iwapo kila mmoja atachukua hatua ikiwamo abiria kutoa taarifa wanapoona dereva anaendesha mwendo usiofaa.

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Natabiri Watanzania watachagua sera



Nkwazi Mhango, Canada

KABLA ya kuzama kwenye mada, lazima niseme wazi. Natabiri kuwa Watanzania watachagua sera na si sura; uzoefu na si uanagezi; uhalisia na si hekaya za Abunuwas; ustaarabu na si matusi; ukweli, si uongo, uhalisia, si uchochezi na matendo na si nadharia.

Kwani urais si nafasi ya majaribio wala tambo bali serious business kwa kisambaa. Mnajua ninachomaanisha hata kama naongea kilevi. Kwa taarifa yenu, walevi wengi ni wasomi na watu wasio wanafiki. Ukimkosea mlevi, kabla hajawa mbwi, atakugwaya. Akishaweka vitu vyake, jiandae kufurumushiwa ukweli unaouma na kuchukiza kinoma. Hivyo, nisemayo leo, ni matokeo ya kanywaji. Waliozoea vitu vilivyotulia na kwenda shule, leo watanshangaa wakidhani sina akili nzuri wasijue mie ni bonge la daktari tena wa falsafa zote. KTY (kwa taarifa yako), hakuna watu wakatili kwenye kutovumilia ghilba kama walevi. Ukitaka kumdanganya mlevi, mnyime kanywaji. Ukitaka ukweli wengi wanaokuficha, mpe mlevi kanywaji.

Nizame kwenye mada sasa. Kuna mchambuzi mmoja kwenye mitandao, amekuwa akisema kuwa uchaguzi huu unaweza kuwa wa aina yake kwa vile wapiga kura watapiga kwa huruma badala ya hekima. Nakubaliana naye kuwa uchaguzi huu ni wa aina yake kwa vile umejaa wabangaizaji hata wachochezi wanaojua kuwa watapoteza, lakini watapata kiki.

Kwanza kwa wanaojua maana ya kufaa katika kutumikia watu, wapiga kura huangalia mambo mengi na si kumuonea huruma mgombea. Wapiga kura si mama au baba huruma.

Pili, kutumia uzoefu wa Nelson Mandela, rais wa kwanza mzalendo wa Bondeni alivyochaguliwa kwa vile alikuwa amefungwa na serikali ya kikaburu kwa jumla ya miaka 27. Ni kushindwa kuelewa kuwa serikali ya kikaburu ilikuwa haramu. Ni kushindwa kuelewa kuwa mateso yatokanayo na kupigania umma. Mandela alipigania uhuru. Siasa za Afrika Kusini na za kipindi kile ni tofauti na za sasa za Bongo ambapo lazima utumie bongo na si bango, sera na si sura, matokeo halisi na si matarajio.

Tatu, kwa kuzingatia kile Watanzania karibu wote wanahitaji wataangalia utendaji wenye mashiko. Katika yote, maendeleo yatachukua kiti cha mbele kwenye vipaumbele ambayo Watanzania wanavyo. Afya, amani, barabara, elimu, miundombinu, nishati, na usalama vitakuwa ni tunu wanazotaka anayetaka kuwaongoza awe na uwezo wa kuwahakikishia ima kutokana dira na ilani yake au mambo ambayo ameishayafanya. Hawatakubali kugeuzwa mabunga wala sehemu ya siasa za majaribio. Huu ni ukweli ambao unaweza kuuapia hata bila kupata kanywaji. We are now going practical as opposed to theoretical. Kwa kimakonde ni kwamba sasa tunaangalia vitendo na si ngonjera na mashairi. Kwa kijita ni chikerebe, cha kwa akina Pius Msekwa, ni kwamba kapira bwacha sugu si salamu bali kanuni ya sayansi.

Amini usiamini. Watanzania wa sasa si wa jana. Wanataka mambo yanayowezekana na si hadithi za Paukwa Pakawa. Siasa siyo hadithi ya mapenzi. Ni uwanja ya maslahi tena mapana na mengi. Ukitekeleza nilichokutuma na ulichoahidi, nani akuondoe? Waliokuwa wakitaka maji wakayapata watamchagua aliyewezesha; kadhalika kwa barabara, umeme na mengine. Waliochukia ufisadi watachagua aliyeuangamiza; ukwepaji kodi na wizi wa rasilimali zao watachagua aliyekomesha kadhia hii. Mwenye macho haambiwi tazama; mwenye masikio sikia. Kila kitu kiko wazi kama usiku na mchana. Nani ni usiku na nani mchana? Usiku ni kiza kitupu. Hujui wala kuona uelekeako zaidi ya kelele za wadudu na vyura. Mchana, kila kitu kiko wazi. Hata ukifumba macho utaona tu.

Ikifika siku ya uchaguzi, chagua uwezekano na si matarajio na ahadi za urongo zisizo na rekodi yoyote ya utendaji. Chagua maendeleo na si maneno matupu. Kwani maneno matupu yanaliwa? Narudia. Mwenye macho haambwi tazama; na mwenye maninga haambiwi tazama. See you.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Jamani shule zetu zikaguliwe basi!



Na Joseph Kulangwa

ZAMANI tukiwa shuleni, shule za msingi, mara kwa mara tukiwa madarasani tulishitukia wakati mwalimu akiendelea kufundisha, akiingia 'mwalimu' mwingine na sisi kulazimika kusimama na kumwamkia "shikamooo Mwalimu" kwa pamoja.

Naye akiitikia "marahabaa hamjambo wanafunzi?" Nasi kumjibu "hatujambooo!" Na kuturuhusu tukae na kuendelea na masomo, huku mwalimu wetu naye akimkaribisha kwa unyenyekevu naye mgeni wetu akienda kukaa dawati la nyuma kabisa.

Ikumbukwe madawati ya nyuma katika madarasa ya wanafunzi wa shule za msingi yalikaliwa kwa kiasi kikubwa na wanafunzi manunda, wale wasiosikia si kwa masikio bali kwa akili, yaani watukutu waanzisha fujo.

Sasa siku ikitokea mgeni huyo kafika na kukaa nyuma, yalikuwa mateso kwelikweli kwao, lakini pia hata mwalimu alionekana kubadilika kitabia, kama alikuwa mkali, siku hiyo aligeuka mpole kupitiliza na kufundisha bila kiboko mkononi.

Bahati mbaya, ziku zote hizo hatukutambulishwa hao 'wale wavamizi' walikuwa ni kina nani mpaka walimu wetu wanoko kupoa kiasi kile, wakifundisha bila kufoka na kutuita majina ya ajabu ajabu ya ng'ombe wewe, mbuzi wewe, nguruwe wewe, na mengine mengi tu.

Kumbe baadaye tukaja kujua kuwa walikuwa ni wakaguzi ambao walifika, kuona hali ilivyo ya kiufundishaji, mahudhurio na mambo mengine yaliyohusu ufundishaji na ujifunzaji. Walikuwa watu muhimu sana kumbe kwetu.

Ndio waliohakikisha kuwa mihutasari iliyopangwa inafuatwa bila vikwazo na walimu wanafundisha kikamilifu na kwa wakati. Walihakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri na kupeleka taarifa ngazi za juu na kama kulikuwa na matatizo basi ufumbuzi wa haraka ulipatikana.

Ndio hao waliopendekeza, mwalimu au mwalimu mkuu aliyefanya vizuri basi apandishwe cheo na kuwa Mratibu Kata kama si Ofisa Elimu. Shule ziliendeshwa kwa mipango mizuri, na kumbuka nyingi zilikuwa za Serikali na ndizo zilizolengwa hasa zikishindana na za Misheni.

Kwa hiyo unyenyekevu feki ule wa walimu wetu ulizingatia kuwa majaaliwa yao yalikuwa mikononi mwa wakaguzi hao, na ndiyo sababu mara walipoondoka, walimu walijivua ngozi za kondoo na kubaki fisi na chui walewale na kutuonesha cha mtema kuni.

Nimeikumbuka hii baada ya siku za karibuni kusikia taarifa na habari za kusikitisha, kuhusu wanafunzi 10 wa shule ya msingi ya kiislamu ya Byamungu wilayani Kyerwa, mkoani Kagera kupoteza maisha kutokana na ajali ya moto bwenini.

Habari za wanafunzi wawili wa shule ya msingi Chilala, wilayani Lindi, kuchapwa na walimu wao na kisha kulazimishwa kutafuna korosho mbichi. Lakini pia kusikia habari kuwa mwanafunzi wa shule ya msingi Maweni, wilayani Chato, Geita, kupoteza maisha baada ya kufunikwa na kifusi akichimba shimo.

Wale wa Kyerwa, yawezekana ni ajali lakini pia yawezekana ni kazi ya mkono wa binadamu. Sijui mpaka tuambiwe na wahusika. Wale wa Lindi haki ya Mungu ni ukatili wa walimu, utawatafunishaje watoto korosho mbichi! Utomvu wa korosho mbichi ni tindikali, unaunguza. Watu wanachorea tattoo miilini kutokana na moto wake.

Wewe mwalimu unaamua kuwatafunisha ili waungue midomo, ili wababuke fizi! Kisha ujiite wewe ni mzazi na kusahau kabisa usemi wa uchungu wa mwana aujuaye mzazi! Unamwunguzia mwenzako mwanawe, halafu unajiita mwalimu mrekebisha tabia ya wanafunzi, tabia yako ikoje?

Huyu wa Chato, pamoja na kwamba ni ajali, lakini kuna mkono wa binadamu. Hivi wewe mwalimu uliyetoa adhabu hiyo, nani alikwambia hakuna adhabu mbadala? Au kwa kuwa udongo huo mlikuwa mnafyatua matofali mnayachoma na kuyauza kwa maslahi ya matumbo yenu?

Na ni bahati mbaya, kwamba wachimbaji wanafunzi, wafyatuaji wanafunzi, wachomaji wanafunzi, wauzaji wanafunzi, lakini walaji walimu! Ukatili na unyonyaji gani huu kwa jina la adhabu? Yote haya yanafanyika kutokana na kukosekana kwa wakaguzi waliokuwa wakituvamia enzi hizo.

Wangekuwapo pengine bweni la Byamungu lingekaguliwa na kasoro kurekebishwa kabla, kifusi kisingechimbwa

## KONA YA UKWELI

# Watanzania, tukapige kura tupate viongozi walio makini



Na Thobias Mwanakatwe

HAPANA shaka, kile kipindi cha Watanzania kuwachagua viongozi wa ngazi za urais, ubunge, uwakili na udiwani kimewadia.

Kuanzia asubuhi hadi jioni ya Oktoba 28, Watanzania nchini kote, wale waliojiandikisha na kuhakikiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na ile ya Zanzibar (ZEC), watasimama kwenye foleni na kupiga kura kuwachagua viongozi wao.

Kwa upande wa Zanzibar, siku hiyo wananchi watapiga kura tano. Ya kwanza, ni ya kumchagua rais atakayeongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na ya pili ni kumchagua rais atakayeongoza Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Wakati ya tatu ni ya kumchagua mbunge, ya nne mwakilishi wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar na ya tano ni ya kumchagua diwani.

Kwa upande wa Tanzania Bara, wananchi watapiga kura tatu-kumchagua Rais wa Muungano, mbunge na diwani.

Upigaji kura huo utakuwa hitimisho la kazi kubwa na ya aina yake iliyofanywa na wagombea wa ngazi zote kwa kipindi cha kampeni cha zaidi ya miezi miwili ya kujinadi wao, sera na ilani za vyama vyao.

Hapana shaka, wengi watakubaliana nami kwamba lengo kuu la kuwachagua viongozi hao ni ili kuwawezesha wakawatumikie wananchi. Hiyo ni pamoja na kuhakikisha wanapambana na maadui wakubwa watatu wa taifa, ujinga, maradhi na umaskini na kuwaletea maendeleo.

Nimeanza kwa kuyaeleza hayo, kwa sababu wapo baadhi ya wananchi ukipita mitaani wanaanza kusema uchaguzi wa mwaka huu hawatashiriki kupiga kura.

Wanaosema hayo ukiwahoji unakuta hawana sababu zozote za msingi na inawezekana kabisa kwamba hawa hawajui kuwa suala la kupiga kura ni haki yao ya msingi.

Hapa naishukru NEC ambayo imezishirikisha taasisi binafsi zisizidie kutoa elimu kwa wapigakura, pengine hili litasaidia kuwaondoa tongotongo wale wanadhani kuwa suala la kupiga kura halina maana.

Katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haki ya kupiga kura imeainishwa katika Ibara ya 5 (1) ambayo inaeleza kuwa; "Kila raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Tanzania na wananchi."

Na haki hii itatumiwa kwa kufuata masharti ya ibara ndogo ya (2) pamoja na masharti mengineyo ya katiba hii na sheria inayotumika nchini Tanzania.

Siku ya kupiga kura, mwananchi kabla hujachukua uamuzi lazima uyatafakari maneno, kauli, ilani na sera ambazo mgombea husika alikuwa akiyanena kwenye mikutano yake ya kampeni.

Na hapa ndipo unatambua kuwa kipindi cha kampeni ni cha muhimu kwa wananchi kuweza kusikiliza sera za wagombea kwasababu hapo ndipo unapata kufahamu mgombea mwenye malengo ya dhati ya kukuletea maendeleo ni nani.

Ni matumaini ya kila mwananchi kuwa alipata fursa ya kuwasikiliza wagombea wote, na niwe wazi wapo baadhi yao sera na mipango yao inatisha kidogo kwa mustakabari wa nchi, sina haja ya kuwaelezea wagombea hao.

Wako watu ambao wanadai wao watachagua mtu siyo sera wala chama, kwa kuwa jambo hilo ni uamuzi wa kila mtu lakini kwa mawazo yangu suala la sera na ilani za chama ni la muhimu sana kuzingatiwa siku ya kupiga kura.

Mfano wako baadhi ya wagombea wamesikika kabisa wakitoa maneno ambayo yanaleta mtazamo kwamba siku watakaochaguliwa tu basi vurugu itakuwa ni sehemu ya utawala wao.

Kwa mtazamo wangu, siku ya kwenda kupiga kura haina tofauti na unapokwenda kutafuta mchumba wa kuoa au kuolewa. Ni kwamba ukifanya kosa itakuwa imekula kwako.

Tukumbuke kuwa viongozi tunaowachagua watakuwapo madarakani kwa kipindi cha miaka mitano hadi 2025, kwa hiyo ukifanya makosa itakugharimu muda wote huo.

Watanzania twendeni tukapige kura tukizingatia kuwa tunakwenda kuchagua viongozi sahihi na makini watakaotuletea maendeleo ya kweli na siyo wenye lengo la kuvuruga amani yetu.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA

# Nguvu ya simu za mkononi katika kujenga, kubomoa ndoa



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

MAWASILIANO ni jambo muhimu katika uhusiano na katika maisha ya kila siku. Mawasiliano yanapokosekana huathiri uhusiano. Hata pale mawasiliano yanapokuwapo lakini yakakosa nidhamu na utaratibu, huweza pia kuharibu uhusiano.

Utafiti unaonyesha kuwa, asilimia 90 ya sababu za kuvunjika kwa ndoa hutokana na mawasiliano mabaya baina ya wanandoa. Wanandoa wanahitaji kufahamu ukweli huu na kujifunza kuishi kwa utaratibu na kuwasiliana vizuri ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima katika ndoa.

Simu za mkononi ni chombo cha mawasiliano na zimerahisisha mawasiliano na zimeleta mapinduzi makubwa katika kuboresha mawasiliano duniani. Pia zimechangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kiwango kikubwa.

Mara nyingi simu zetu haziko mbali nasi. Watu wengi tunazo simu wakati wote. Simu za mkononi zimechukua maisha yetu na sehemu kubwa ya muda wetu. Tunaziangalia na kuzitumia mara kwa mara. Ni uhusiano ambao unaonekana kuwa utadumu kwa muda mrefu, hivyo, nidhamu binafsi inahitajika katika matumizi yetu ya simu. Simu za mkononi ni chombo kizuri na muhimu. Utafiti unaonyesha kuwa, ndicho kifaa cha elektroniki kinachouzwa kwa wingi zaidi duniani. Pamoja na mazuri mengi ya simu za mkononi, simu hizi zimeleta matatizo katika ndoa na kuvunjika kwa uhusiano. Simu zenyewe si tatizo, bali watumiaji. Simu inaweza kusababisha changamoto nyingi katika uhusiano kutegemeana na mtu anavyoitumia. Baadhi ya wanandoa wamekuwa wasaliti katika ndoa zao kutokana na matumizi ya simu. Simu zimetumika kupanga mipango ya udanganyifu katika uhusiano. Zimeondoa uaminifu, upendo, na ukaribu wa wanandoa.

Kwa wengine, simu za mkononi zimeboresha na kuimarisha uhusiano wao na kuwafanya wanandoa kuwa karibu zaidi kutokana na uaminifu na kujengeka kwa tabia ya uwazi na ukweli miongoni mwao.

Mawasiliano yanaweza kuboreshwa na kuendelezwa. Kama kweli wanandoa wamejitoa kwa ajili ya ndoa na familia, kila mmoja atafanya jitihada katika kujifunza namna bora ya kutumia simu yake ya mkononi. Matumizi mazuri ya simu na mawasiliano mema huepusha migogoro isiyo ya lazima katika ndoa.

Mwanandoa kuzama katika simu yake wakati mwenzi wake anamhitaji au anapenda kuzungumza naye ni dalili ya kutokujali na kutokuthamini. Kumbuka, kumpa mwenzi wako muda na kumsikiliza ni kuonyesha upendo kwake na namna ya kueleza kwamba unajali na kuthamini.

Kutokana na ukweli huo, mwanandoa unapaswa kujiuliza na kutafakari maswali haya; je, una uhuru na simu ya mwenzi wako? Unaruhusiwa kuishika au kuitumia? Unaweza kupokea simu inapopigwa katika simu ya mwenzi wako pale anapokuwa hayuko karibu na simu yake? Ukipigiwa simu na mtu wa jinsia tofauti wakati ukiwa na mwenzi wako, unajisikia amani moyoni mwako kuongea mbele yake? Kati ya simu na mwenzi wako, kipi kimechukua nafasi kubwa zaidi kwako?

Je, una muda na mwenzi wako? Umewahi kugombana na mwenzi wako kwa sababu ya matumizi ya simu yako? Ulichukua hatua zipi? Je, kiwango cha mawasiliano na mwenzi wako kwa njia ya simu kimeongezeka au kimepungua? Unadhani kwa nini? Simu yako ina nywila (password)? Kama ndiyo, Je, Mkeo au mumeo anaijua nywila hiyo? Kama haijui, unadhani kwa nini? Maswali haya yakusaidie kujitathmini katika suala zima la matumizi ya simu yako/zako.

Mawasiliano ya simu yametajwa kuwa chanzo cha ndoa nyingi kuvunjika. Utafiti na uzoefu wangu katika mashauri ya ndoa vinaonyesha kuwa, kukosekana kwa uaminifu na heshima miongoni mwa wanandoa imekuwa chanzo kikubwa cha matatizo katika ndoa nyingi. Wanandoa wengi, kama ilivyo kwa watu wengine, hawafahamu maadili ya simu kwani simu hizi za mkononi kwa bahati mbaya zilikuja na kuanza kutumika kabla ya watu kupata semina juu ya matumizi yake.

Baadhi ya wanandoa wamekuwa watumwa wa simu zao. Wengi hawana nidhamu ya matumizi ya simu zao. Hawajui mahali na wakati unaofaa au usiofaa kutumia simu. Imetokea mahali pengine kwamba mke na mume wakiwa katika mapumziko ya pamoja, matembezi, faragha au nyumbani, kila mmoja au mmoja wao anakuwa amezama katika simu yake muda mwingi kuliko kupata muda na mwenzi wake.

Mwenzi anajali zaidi simu yake kuliko uhusiano wake na mumewe au mkewe, hivyo, kuwa mtindo wa maisha. Simu ya mkononi imekuwa kama mke au mume wa pili.

Simu ya mkononi ni chombo binafsi cha mawasiliano na sheria ya mawasiliano nchini inamlinda mtumiaji. Mtu anaposajili simu au kadi ya simu, atasajili kwa jina lake binafsi kwa kutumia kitambulisho chake cha Taifa na kuweka alama za vidole vyake.

Hii ndio kusema kuwa, yeye ndiye mhusika mwenye dhamana na simu au kadi hiyo. Pale litakapotokea tatizo kuhusiana na simu hiyo, atakayewajibika ni mwenye simu hiyo. Kwa kuwa simu ya mkononi ni chombo binafsi cha mawasiliano, ni wazi kuwa simu imejaza taarifa nyingi binafsi za mtu.

Kwa mantiki hiyo, mume au mke kutamani kupekua pekua simu ya mwenzi wake ni kumkosea mumewe au mkewe, kwani kufanya hivyo ni kuingilia uhuru wa mtu mwingine katika matumizi ya simu yake. Aidha, hii ni dalili ya wanandoa kutokuaminiana.

**Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare) inayojihusisha na masuala ya Ndoa na Malezi ya Watoto. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye Kwa: info@tamcare.or.tz"**


# MAISHA

SEPTEMBA 27, 2020

Nipashe


Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



**HARUSI**

Ukurasa 12



Ukurasa 10

**Usimkatishe tamaa, msaidie aelewe**



## MAISHA NI NYUMBA

Jiko ni zaidi ya sehemu ya mlo

Ukurasa 15



**Chapati za maziwa na siagi**

Ukurasa 14




'SIX PACKS'

# Mikato yenye maajabu

Ukurasa 14

# Usimkatishe tamaa, msaidie aelewe

**Na Moses Ismail**

NI mtoto wako mdogo, ana miaka 11 pengine, lakini ni mzito kuelewa haraka chochote kile anachofundishwa darasani na walimu wake kwa sababu hiyo matokeo yake shuleni yanakuwa mabaya kila mara.

Inatokea rafiki zako wamekutembelea nyumbani, mmoja wao anaamua kumuuliza mtoto wako; "wewe unataka usome mpaka darasa la ngapi?"

Kwa hofu, mtoto wako anakuangalia kwa kiwogawoga, kisha anajibu swali hilo huku akiwa ameinamisha uso wake chini: "Mpaka 'fomo siksi'."

Kama alivyotegemea mtoto huyo, wewe mzazi unaingilia kati na kusema: "'Fomu siksi' unafikili mchezo. Mjinga kama wewe unaweza kufika huko, utaishia darasa la saba tu na wala sitoi hela yangu kukusomesha ukifeli."

Unaposema hayo sauti yako inaonyesha hutanii, umedhamiria, na hapo ndipo mtoto wako anapoanza 'kushikashika' vidole vyake vya mikono na kisha kuondoka sebuleni kichwa chini huku machozi yakimlenga.

Amezoea kusikia kauli hizo toka kwako na pengine hata kwa mama yake na wadogo au kaka zake, kila anapoonyesha kuwa ana ndoto au mtazamo fulani wa kufanya kitu kikubwa siku za usoni, anakatishwa tamaa na kubezwa.

Hili, la kukatishwa tamaa na kubezwa, linatokana na uzito wake wa kuelewa masomo na hata mambo mengine ya kwaida anayofundishwa au kuambiwa, mzito sana kuelewa na inamchukua muda mrefu kuelewa jambo dogo tu.

Kwa sababu hiyo anaingiwa na 'moyo' wa kukata tamaa na kujiona kuwa yeye ni mtu asiyeweza jambo lolote lile na hilo linamuumiza zaidi kila anapokumbana na hali ya kuzodolewa na anakuwa mnyonge na asiyejiamini kwa lolote.

Lakini kwa nini mtoto huyu amekuwa mzito kuelewa? Hivi, hakuna mbinu wala 'tiba' ya kumbadilisha na kumfanya awe kama watoto wenzake wa umri wake wanaoelewa mabo ambayo yeye ameshindwa kuyaelewa?

Mtaalamu wa masuala ya saikolojia ya watoto, Denis Munga, anatoa majibu ya maswali hayo. Anasema:

"Kwanza ifahamike hakuna mtoto asiyeelewa wala asiyefundishika, ila wapo watoto wazito wa kuelewa wanaochukua muda mrefu kuelewa, unaweza kuwaita 'slow leaner', na kuna sababu nyingi zinazowafanya wawe hivyo zikiwemo za kimaumbile ya ubongo.

"Hawa ni watoto wanaohitaji msaada maalumu toka kwa wazazi na walimu. Wanahitaji msaada huo kwa sababu tatizo lao la uzito wa kuelewa linahitaji mwalimu anayewafahamu kama mtoto anatatizo hilo na ajue mbinu za kulikabili.

"Lakini njia nyepesi zaidi na ya msingi, ambayo haihitaji mzazi au mwalimu awe na elimu ya kuwafundisha watoto wa aina hii, ni kuwapa moyo. Hawa wanahitaji upendo katika kufundishwa na kuambiwa kuwa wanaweza ila wakijitahidi kidogo tu!"

Inawezekana kuwa una mtoto wa aina hii na anakuudhi kweli, ila kumchukua au kumsema hakuwezi kumsaidia bali kutamfanya awe mzito zaidi, badala yake jaribu kumpa moyo huku ukionyesha upendo mkubwa kwake. Ataelewa tu!

## NA KHAMIS KIDAGO

0657 207168

# QUIZ

**LE QUIZ DU WEEK – END**

1. Weka sentensi zifuatazo katika wingi.
   Mfano: Une course incroyable – Des courses incroyables.

a. Un résultat très décevant

......................................................

b. Un relais victorieux

......................................................

c. Une championne olympique

......................................................

d. Un record battu

......................................................

e. Un prix exceptionnel

......................................................

f. Un saut extraordinaire

......................................................

g. Un titre précieux

......................................................

h. Un prix special

......................................................

i. Une récompense méritée

......................................................

j. Un château feudal

......................................................

k. Un bureau central

......................................................

l. Un point capital

......................................................

m. Un geste amical

......................................................

n. Un détail spécial

......................................................

o. Un test final

......................................................

p. Un travail original

......................................................

q. Un vent glacial

......................................................

r. Un scénario banal

......................................................

s. Un festival international

......................................................

2. Malizia sentensi zifuatazo kwa kuweka article le, la, l' au les.

- De quelle couleur est...... drapeau(m) français?
- Comment s'appelle.....(m) président de.....(f)République française?
- Qu'est – ce que....Élysée(m)?
- Quelle est....date de....(f)Fête nationale?
- À quelle fête sont associés.....(m)œufs en chocolat?
- Qu'est – ce – que........ impressionisme(m)?
- Où se trouve.....(f)embouchure de......(f)Seine?
- Quelles sont........(f)cinq plus grandes villes françaises?
- À quel département correspond....(m)code postal 75006?
- Quelle est.....(f)vitesse maximum du TGV?

### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA

1. Badili nomino zifuatazo za kifaransa kuwa vitenzi kwa kifaransa.
   Mfano: Unemploi – Il emploie.

- Un travail – Il travaille
- L'ennui – Il ennuie
- Un entretien – Il entretient
- Un envoi – Il envoie
- Un essai – Il essaye
- Le flair – Il flaire
- Le gel – Il gele
- Le maintien – Il maintient
- L'oubli – Il oublie
- Un pari – Il parie
- Un pli – Il se plie
- Le rappel – Il se rappelle
- Le recours – Il recourt
- Le recul – Il recule
- Le réveil – Il se réveille
- Un salut – Il salue
- Un signal – Il signale
- Un souci – Il se soucie
- Le soutien – Il soutient
- Le tri - Il trie
- Le cri – Il crie
- Un trou – Il troue
- Un vol – Il vole
- Le viol – Il viole
- Un zigzag – Il zigzague

2. (Viable) au (vivable)?
¬ Le métier de professeur n'est pas vivable financièrement.

3. (Conjoncture) au (conjecture)?
¬ Se perdre en conjectures

4. (Prodige) au (prodigue)?
¬ Joseph est un enfant prodige

5. (Prescrire) au (proscrire)
¬ La vente de cigarettes aux mineurs est proscrite par la loi.

6. (Notable) au (notoire)?
¬ Une perte notable

7. (Comprénsif) au (compréhesible)?
¬ Mon père a été Comprénsif sur le fait que je ne souhaitais pas faire le même métier que lui.

8. (Affectation) au (affection)?
¬ Ce chien est d'une affection sans bornes pour son maître.

9. (À l'attention de) au (à l'intention de)?
¬ Une lettre à l'attention de Bob Rasha.

10. (Près de) au (prêt à)?
¬ Il n'est pas près d'y arriver.


11. (Allocation) au (allocution)?
¬ Son allocution n'a pas convaincu les électeurs.

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA KIDOGO



Alichokifanya daktari

Doktari mmoja alikwenda kula na kumuacha msaidizi wake aendelee kutibu wagonjwa.

Aliporudi alianza kumhoji msaidizi wake

Doktari: uliwaona wagonjwa wangapi?

Msaidizi: " Nliwashughulikia wagonjwa watatu, mmoja aliumwa kichwa nikampa panadol"

Doktari: "Safi sana, na wa pili?"

Msaidizi: "Wa pili alikuwa anaumwa na tumbo, nikampa flagyl"

Dokta: " safi sana, na watatu je?

Msaidizi: Alikuja mtu amevurugikiwa akili, nikampa dawa ya matone ya macho"

Dokta: "Tobaaaa?"

===================

**SWALI**

Mnyama mwenye shingo ndefu anaitwaje?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mume wangu kanichosha kwa uhusiano nje ya ndoa, nashindwa kumwombea!

ENZI msomaji, karibu tena tuendelee na vimbwanga vya safu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo.
Ndoa nyingi zina majeraha yasiyopona kirahisi hadi kukatisha tamaa.
Lakini ukweli uko pale pale kwamba ni safari ndefu. Kuna wakati wa kufurahi na kuna nyakati zitawalazimu kulia.
Kuna wakati mtapishana katika kufanya uamuzi.
Vile vile kuna wakati uchumi utashuka katika maisha na wakati wa mawazo kugongana na mmoja wenu aweza kuugua.
Na hapo ndipo upendo wa kujitoa unatakiwa kudhihirika kwa kila mmoja.
Ndoa inaweza kusimama tu pale wanandoa watakapokuwa wamoja na upendo wa kweli kama vile Mungu alivyotukirimia pendo lake tangu kuumbwa wa ulimwengu. Ndoa ni agano linalowaunganisha watu wawili kuishi kwa umoja. Kiunganishi hiki kinapokatika, tayari ndoa inatikisika.
Mpenzi msomaji, pamoja na ukweli huo, ndoa nyingi zinaandamwa sana na maadui.
Hawa wanaweza kuwa ndugu wa karibu, majirani, marafiki na kadhalika. Maandiko ya Mungu yanasema, adui wa mtu ni wa nyumbani kwake. Ni yule mtu aliye karibu yako.
Hebu sasa msomaji nikujuze kilio cha mama huyu kwa yale anayopitia katika ndoa yake.
Mume wake amesaliti ndoa akidhani lilikuwa jambo la muda kumbe amenaswa na kahaba, hawezi kujinasua.
Mama huyu kwa uchungu mkubwa akanitumia ujumbe ufuatao kupitia simu ya kiganjani.
Anasema hivi: "Mimi ni mhanga wa usaliti. Nimeokoka na pia namwombea sana mume wangu lakini suala la usaliti halijawahi kuisha.
"Tumeishi miaka 14 ndani ya ndoa, lakini bado mume wangu haachi kutafuta wanawake wengine. Naumia sana, nashindwa hata kuendelea kumwombea.
"Kuna kipindi alimwambia mwanamke wake kuwa mimi nimemwachia watoto na kwenda kuolewa na mwanaume mwingine.
"Hivi karibuni wiki mbili zilizopita niliamua kuondoka kutokana na kuwa alifikia hatua akaanzisha mahusiano na mfanyakazi wangu wa nyumbani. Akamwambia eti anatafuta furaha nje ya ndoa. Nimekaa na maumivu sijui yataisha lini.
"Nikimuuliza mume wangu nina tatizo gani, anaishia tu kusema nisamehe mama, niombee!
Samahani kwa usumbufu. Ni vile tu nimefikia mahali nashindwa hata kuendelea kuomba. Sijui niombe kwa namna gani.
"Nafika mahali, hata akiniambia twende kanisani nakuwa na wakati mgumu mno. Kwa kifupi najiona kuwa sina nguvu ya kuendelea mbele, japo najiambia siwezi kuishia hapa.
Mpenzi msomaji, bila shaka umemsikia vyema mama huyu kwa yale anayopitia. Ninachokiona haraka ni kwamba baba huyu ametekwa ufahamu na mahusiano nje ya ndoa.
Siku ile aliposaliti ndoa yake na kutafuta wanawake nje, ndipo alipobomoa ndoa yake. Mpasuko wa ndoa huanzia ndani. Mmoja wa wanandoa anapotafuta uhusiano nje, tayari amepanda mbegu ya mafarakano na kupoteza thamani ya ndoa.
Nimejaribu sana kumshauri mama huyu awe mtulivu na azidi kumsihi Mungu amnasue mumewe katika hicho kifungo cha makahaba. Hata hivyo, si kwamba Mungu hawezi kuponya ndoa hiii, kwani Mungu ni wa kanuni.
Mama huyu anasema yeye ni mwombaji sana. Lakini pengine kuna eneo hajalifanyia kazi vile ipasavyo. Kwa mfano, anapaswa kujiombea rehema kwa yale aliyowahi kufanya ambayo ni chukizo mbele za Mungu.
Pia amwombee rehema mumewe kwa hizo roho zinazomwingia hata kuisahau familia yake na kuambatana na wanawake wa nje. Dhambi ndiyo chanzo kikuu cha matatizo mengi yanayowakumba wanadamu. Ndiyo maana kabla ya kuomba chochote kwa Mungu lazima kwanza kuomba rehema, ndipo akusikilize.
Wako watu wengi wamefanya dhambi kama vile kuua hata kama ni kwa kujua au kwa bahati mbaya, wameshiriki mambo ya kichawi na kiganga na kadhalika. Pia watu wengi watateseka ndani ya ndoa kwa sababu hawakumshirikisha Mungu tangu mwanzo.
Ukimshirikisha Mungu, atakuchagulia mtu sahihi kabla ya kuoa au kuolewa. Wako wanaoteswa na wenzi wao kwa kutokuwa makini pale wanapokutana mara ya kwanza. Wanakurupuka, wanaoana kumbe tabia zingine zimejificha. Matokeo yake wanashindwana mbele ya safari.

**Maisha Ndivyo Yalivyo. Mpenzi msomaji, niishie hapa ili nawe utoe maoni, ushauri au pia ulete kisa chochote tujadili pamoja. Ukiwa tayari tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581. Namba hii ipo pia WhatsApp . Tukutane wiki ijayo.**

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Kampuni za wasichana wa kazi zitupiwe jicho

NI kawaida kwa familia nyingi kuwa na wasichana na vijana wa kazi za nyumbani na kila mmoja hutafuta kwa namna anavyoweza kupata. Wako ambao hutafuta kwa kuunganishiwa na ndugu, rafiki na watu wengine na ndipo kunakuwa na maelewano baina ya anayetaka kufanya kazi na mwajiri.
Baadhi ya watu wameona ni fursa na kufungua kampuni za kutafuta wasichana kutoka mikoa mbalimbali na kuwapeleka katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Dodoma, kuwafundisha na kuwakabidhi kwa familia mbalimbali kulingana na makubaliano yanayowekwa baina ya pande zote.
Baadhi wanafanya kazi hizo kwa kufuata taratibu zilizopo ikiwamo kusajili, kuwatafuta mabinti wanaotafuta kazi kuwafundisha na baadaye kuingia mkataba baina ya pande tatu (msichana, mwajiri na kampuni). Kwa baadhi ya kampuni taratibu zinazofanyika ni anayepewa msichana kulipa Sh. 100,000 kama nauli ya kumpeleka binti na kuwa na masharti ya kufanya kazi katika nyumba husika kwa miezi mitatu kabla ya kuondoka. Kipengele kingine ni kuhakikisha akivunja mkataba halipwi mshahara unarudi kwenye kampuni ambayo ina wajibu wa kutafuta msichana mwingine.
Baadhi ya masharti yanayokuwapo kwenye makubaliano ni kutohusika na wizi, lakini imekuwa tofauti kwa kuwa baadhi wanatumika kufanya wizi kwenye familia husika na kampuni hukana kujua wanakotoka.
Masharti mengine ni kumpa ruhusa ya saa 24 kwenda kuona ndugu zake kama anaye anayeishi mji husika, na mwisho wa mwaka ni lazima kumpa likizo ya mwezi mmoja.
Kampuni hizo hujinasibu kuwa zinawafundisha wasichana hao mapishi, usafi na majukumu mengine ya nyumbani, lakini kinachoendelea ni kuwahamisha kutoka nyumba moja kwenda nyingine.
Baadhi hufanya kwa uaminifu ila wengi wameingia tamaa na sasa kinachofanyika ni udanganyifu ambao sasa unaharibu kabisa waliona jambo hilo kama ni fursa na kuitumia na kugeuka kuwa manyanyaso kwa wasichana na wanaotafuta wasichana.
Mathalani, mtu anapoingia makubalino na kampuni husika msichana anapokuwa mzuri anayetekeleza majukumu yake vizuri na akiwa amemaliza miezi mitatu ya lazima ya mkataba, visa huanza kuanzia mwezi wa nne na baadaye huondoka bila sababu.
Kinachofanyika ni kutafuta namna ya kumuondoa na kumpeleka kwingine ili wapate malipo ya Sh. 100,000 ya kuingia makubaliano mapya, jambo ambalo halipaswi kuwa hivyo, na wanafanya hivyo kwa kuwa ni faida kwao wanapata hizo fedha mara kwa mara.
Kwa sasa wasichana hawa wamejikuta wakimangamanga kwenye nyumba za watu kwa kuwa wanaondolewa kwa shinikizo la aliyemtafutia kazi, jambo ambalo linaonyesha wanatumiwa kwa maslahi ya wachache wenye kampuni husika.
Ni muhimu sana kwa jamii sasa kuamka juu ya hiki kinachofanyika ambacho kinaleta sura ya namna ya kujipatia fedha kwa namna ambayo siyo sahihi kabisa.
Hakuna ubishi familia zinahitaji wasaidizi wa nyumbani kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali, ikiwamo kuangalia watoto wakati wanafamilia wakiwa kazini, na ndiyo maana wengi wanatafuta kwa kampuni ili kuhakikisha wanapata watu wa uhakika.
Inapotokea sasa wengine wamegeuza jambo hilo kama namna ya kupata fedha kwa haraka inapoteza maana na uamunifu kwa kampuni zinazofanya kazi hizo.
Ipo haja kwa mamlaka mbalimbali kufuatilia hizi kampuni zinazoleta wasichana kutoka vijijini kuja mjini, kama zinafuata taratibu au zinakusanya fedha na kujihusisha na ubabaishaji.
Wapo watakaoishia mikononi mwa watu wenye utu lakini wapo aambao watafanya mambo yasiyofaa na matokeo yake kuwa hasara kwa msichana au familia husika.
Mathalani hao wanaoiba ni hatari zaidi kwa kuwa kama wanaiba ndani ya nyumba, maana yake ni rahisi kushirikiana na vibaka, wezi na majambazi kuiba kwenye familia za watu, au wengine kutumika kuchora ramani kwenye familia za watu.

**Mungu Ibariki Tanzania**
**Kwa maoni, Ushauri: salomekitomari33@gmail.com**



# Nikas & Prisca

Ilikuwa siku ya furaha kwa Nikas Meinkya na Prisca Mwanjesa baada ya kufunga ndoa katika Kanisa la KKKT Mburahati, Agosti 1, 2020 na kufuatiwa na sherehe iliyofanyika kwenye bustani ya nyumbani kwa wazazi wa bwana harusi, Mikocheni, jijini Dar es Salaam

MITINDO



# TUPIA KINIGERIA UTAPENDEZA

MITINDO ya mavazi ya Kinigeria imekuwa maarufu katika bara la Afrika, Watanzania ni miongoni mwa kundi la watu wanaoleweshwa na mavazi yenye asili ya nchi hiyo.

Katika sherehe za harusi, hafla za kiserikali na sehemu za burudani, utaona watu wa jinsia zote wamevaa nguo za aina hiyo, huku wakionekana zimewatoa sana.

Kiujumla, mavazi haya yanayofahamika kama E aso Ebi, yalikuwa yanavaliwa na jamii ya Yoruba kutoka Magharibi mwa Afrika kati ya miaka 1960, 1970 na 1980.

Lakini kutokana kukua kwa teknolojia, kila wakati mavazi hayo yanabadilika muonekano wake, kiasi ambacho watu kutoka nchi mbalimbali wanavaa kulingana na mtindo anaotaka.

Wabunifu nao hawako mbali, kwani kila siku wanafikiria namna ya kuliboresha kiasi ambacho hata muonekano wake umebadilika na kuwa wa kisasa zaidi.

Vazi hili linaloambatana na gauni refu au la wastani, linakamilika kwa mwanamke kama akivaa kilemba maalum chenye umbo la uyoga kichwani, huku upande mmoja kitambaa ukiwa umetupiwa begani.

Kwa mwanaume, anaweza kushona kanzu pana na ndefu, au kanzu fupi na suruali ya kitambaa, huku kichwani akiwa amevaa kofia maridadi inayofanana na nguo yake.

# UREMBO

## 'SIX PACKS' Mikato yenye maajabu




WAREMBO wa sasa huwa hawaoni wala hawasikii, pale wanapokutana na mwanaume ambaye emejengeka misuli ya tumbo na kumfanya aonekane kuwa na mikato.

Mikato hii ya tumbo maarufu kama 'Sixpacks' inatokana na mtu kufanya mazoezi maalum yanayoimarisha misuli ya tumbo.

Kulingana na wataalamu wa urembo, 'Sixpacks' licha ya kumfanya kuwa mvuto tofauti kwa mwanamume, pia wanawake wengi wanavutiwa nayo.

Pamoja kuwa ni matokeo ya mazoezi, lakini katika suala la urembo limewekwa kipaumbele zaidi hasa kutokana na wanawake kuvutiwa nayo.

Misuli ya tumbo imegawanyika katika sehemu kuu tatu, tumbo la juu, tumbo la pembeni na tumbo la chini. Hivyo mgawanyiko huo wa misuli hugawa tumbo pande kuu tatu inayovutia.

**UMUHIMU WAKE**

Hakuna uthibitisho wa moja kwa moja faida za kuimarisha misuli ya tumbo, lakini kiafya inaweza kusaidia mtu kutokuwa na kitambi au kuongezeka mwili haraka.

Pia muonekano wa mtu huwa mzuri, kiasi ambacho kila vazi analovaa linampendeza.

Wasanii mbalimbali wanafanya mazoezi ya kuimarisha misuli ya mwili kama Diamond Platnumz, Ali Kiba na Harmonize.

Kutokana na umuhimu wake, tunaelezea aina ya mazoezi yanayoweza kukupa matokeo ya haraka kujenga misuli ya tumbo.

**TUMBO LA JUU**

Haina hii ya mazoezi hutoa matokeo ya mapema, mtu anatakiwa kulalia mgongo na kisha kukunja magoti bila visigino kugusa chini.

Kisha mikono yako shikilia kichwa kwa nyuma, halafu inuka na kurudi chini mara kadhaa,

unatakiwa kutumia dakika 10 hadi 15 kwa mizunguko miwili hadi nne.

Zoezi lingine unatakiwa kulala ukitazama juu, kisha miguu ikunje huku visigino vikigusa chini.

Nyoosha mikono nyuma ukiwa umelalia mgongo, nyanyuka mpaka usawa wa magoti na kuridi chini mara kadhaa.

**TUMBO LA KATI**

Mazoezi ya tumbo la kati ni pamoja na kulalia mgongo, halafu nyoosha mguu mmoja mbele na mwingine juu bila kisigino kugusa chini.

Unatakiwa kupishana miguu, mmoja ukiunyanyua, mwingine unakwenda chini.

Pia unaweza kufanya zoezi lingine la kulalia gongo, halafu nyoosha miguu yote miwili mbele na mikono mbele ili kuleta usawa.

Nyanyua miguu yote miwili juu na kuishusha chini bila visigino kugusa chini.

Mzoezi mengine yale ya kukaa chini, kasha kiwiliwili chote kinageuka kulia na kushoto, hii ni kwa ajili ya kuimarisha misuli ya pembeni.

# MAPISHI

## Na Mary Geofrey

## CHAPATI ZA MAZIWA NA SIAGI



**Mahitaji**

ANDAA vikombe viwili vya unga wa ngano, vijiko viwili vya unga wa kusukumia na robo tatu ya kijiko kidogo cha chumvi.

Weka vijiko vitatu na nusu vya siagi, robo tatu ya kikombe maziwa na siagi ya kukunjia na kukaangia.

**Namna ya kuandaa**

Changanya siagi vijiko viwili vikubwa na maziwa na chemsha mpaka iyeyuke, maziwa yatakuwa ya uvuguvugu.

Usipotumia microwave, weka kwenye sufuria ndogo na chemsha dakika moja hadi mbili mpaka siagi iyeyuke.

Changanya unga wa ngano, chumvi na mchanganyiko wa siagi na maziwa na kanda mpaka unga ulainike vizuri.

Funika bakuli kwa kitambaa kisafi au nailoni za kufunikia chakula, acha unga upoe kwa dakika 30.

Kanda unga tena, ugawanye kwenye madonge manne yaliyolingana na weka madonge ya unga kwenye sehemu iliyonyunyiziwa unga, funika acha kwa dakika chache.

Sukuma kila donge hadi liwe jembamba kama chapati au zaidi na paka upande wa juu siagi kiasi iliyoyeyushwa.

Kwa kutumia kisu kikali, katakata unga vipande vyembamba sana kwa urefu, ukikata vyembamba zaidi chapati inachambuka zaidi.

Kusanya vipande vyote pamoja kwa ajili ya kukunja vuta taratibu kufanya uwe mrefu zaidi kiasi uanze kukunja utengeneze umbo kama la koni.

Dumbukiza ncha ya mwisho katikati kwa ndani ili isifunguke na acha tena kwa dakika chache unga upumue.

Bandika kikaangio jikoni na anza kupika chapati kwa kupaka siagi juu ya chapati upande uliopikwa.

Geuza tena upande mwingine, paka tena siagi na geuza tena pande zote mbili hadi chapati ziive vizuri, ziwe na rangi ya kahawia ila zisikauke.

Chapati zako zitakuwa tayari kwa jili ya kuliwa kwa chai, maini, nyama au supu.



# MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

# JIKO NI ZAIDI YA SEHEMU YA MLO



NYUMBA iliyokamilika siku zote ni lazima iwe na 'vikolombwezo' vinavyojumuisha vitu vingi vya msingi. Jiko zuri ni lile lililosheheni mahitaji yote, ikiwamo sehemu ya kutolea mvuke/moshi.

Jiko la kisasa linatakiwa kuwa na nafasi ya kutosha ambayo mtu anaweza kuweka kila kinachohitajika bila kubanana.

Rosemary Kwinuka, mtaalamu wa eneo hilo anashauri kuwa na jiko bora na la kisasa ni kujengwa kwa kuzingatia ukubwa wa chumba na mahitaji ya familia.

Pia, anasema ukubwa huo wa jiko unategemea wingi au idadi ya watumiaji wa jiko husika, akiwa na ufafanuzi: "Katika maisha ya kawaida, nyumba yenye vyumba vitatu inahitaji kuwa na angalau na jiko ambalo linaweza kuzungukwa na watu watatu kwa wakati mmoja, angalau liwe na ukubwa wa mita tatu au mbili na nusu.'

Kwinuka anasema ukubwa huo, ndio unaofaa kujengeka vizuri na kwa ubora kulingana na ukubwa wa vifaa vyenyewe.

"Nasema hivyo kwa sababu 'kabineti' ambazo zinatumika katika kutengenezea jiko, nyingi huwa zinaanzia kwa sentimeta 60 kutoka ukutani, halafu urefu wake unakuwa sentimita 90 kutoka chini. Kwa hiyo, kabla ya kuanza kulitengeneza, ni vizuri ukamwita mtaalam ili akushauri na achukue vipimo.

"Katika hili, pia kuna baadhi ya watu huwa wanakurupuka na kujikuta wanajilaumu baadaye, kila kitu ambacho unatumia gharama ni vyema ukatumia wataalamu wanaoeleweka."

# MPANGILIO

# DONDOO ZA NAMNA YA KUWEKA SAHANI, VIJIKO NA UMA KABLA NA BAADA YA KULA CHAKULA.

1; Kabla hujaanza kupata chakula, hakikisha sahani yako ipo wazi, ikiwa pembeni kuna uma, kisu na kijiko.

2: Hakikisha kuna kitambaa jirani cha kujifutia baada ya kula mlo wako.


3: Vijiko, uma na kisu viwe karibu na sahani ili kuepuka usumbufu wa kutembea sehemu moja hadi nyingine kutafuta.

4: Unapokula hakikisha unatumia vizuri vifaa vyako, kijiko utakitumia kuchukua chakula na kuingiza mdomoni. Uma utatumia kuchukulia vitu vigumu kama nyama na saladi na kisu utakatia vipande vya nyama ili utafune kwa urahisi.

5: Ukimaliza mlo wako, hakikisha vifaa vyote unaviweka ndani ya sahani ili kuchuliwa kwa ajili ya kuoshwa.

6: Jifute mdomo na shemu nyingine iliyochafuka kwa kutumia kitambaa kilichowekwa mezani.




KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2020
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
Hivi kwa nini 'TUMEKATAZWA' Kubebana?
Wanajua mimi wa chini nikipiga MWELEKA wewe wa juu utapata 'AJALI MBAYA'
Usikate tamaa. maji ukiyavulia nguo, lazima uyaoge...
Bwanaweee... INATEGEMEA! Kila Mkutano wanajaa watoto kama nagawa 'AISIKRIMU'
Kampeni za safari hii zinakondesha! Nashangaa bado unene ninao! KWANI WANANCHI WANATAKA NINI?
Wanataka KAZI Sio NGONJELA... Utajikuta peke yako UNABWABWAJA!
Unachotakiwa kufanya ni kumwaga Sera na Kutandaza ILANI yako...
Kila eneo ninalokwenda 'NIKIMWAGA' Najikuta nazoa mwenyewe!
'LAHAULAAAAAAH!!! MUDA WOTE JUKWAANI "NIMEPIGA SOGA" NIKASAHAU KUOMBA KURA!...Lakini sio mbaya sikuwa na 'Nondo zaidi ya kusifu Jitihada...
Unajua Kampeni sio kama BOMU ukilipua unayaona matokeo yake... 'KAZA BUTI'
NIMEKAZA KUMBE KAMBA 'ZIMEOZA'
Ni matokea ya kutelekeza JIMBO LANGU toka wani-chague
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UKIPENDWA RINGA KIDOGO...

HABARI KIMATAIFA

# Papa Francis chanzo kadinali kujiuzulu

**ROMA, Vatcan**

KIONGOZI wa kanisa la Katoliki duniani, Papa Francis, amebariki kujiuzulu kwa Kadinali, Giovanni Angelo Becciu, ambaye alichukua hatua hiyo juzi.

Kadinali Becciu (72), alijiuzulu ghafla baada ya kushukiwa kutoa fedha ya kanisa na kuwapa ndugu zake, lakini mwenyewe alikanusha tuhuma hizo.

Becciu alikuwa mshauri wa karibu wa papa na awali alikuwa katibu wa kanisa hilo katika makao makuu yake yaliyopo Vatican.

Alidaiwa kuhusika na mkataba tata wa uwekezaji wa jengo la kifahari jijini London kwa kutumia fedha za kanisa hilo.

Kiongozi mwenye cheo cha Kadinali ni jambo la nadra kuchukua uamuzi kama huo.

"Baba mtakatifu amekubali maombi ya kujiuzulu yaliyowasilishwa na Mwadhama Kadinali Giovanni Angelo Becciu," ilisema taarifa iliyotolewa jana na ofisi ya Papa Francis.

Kadinali huyo, aliuambia mtandao wa Domani nchini Italia, Papa alimlazimisha kujiuzulu kwa sababu alihusishwa na tuhuma ya kutoa fedha za kanisa kwa ndugu zake.

"Sijaiba hata euro moja. Sijafanyiwa uchunguzi, lakini wakinipeleka mahakamani nitajitetea mwenyewe kuwa sijaiba," Kadinali huyo alinukuliwa akisema.

Hata hivyo, alieleza Papa alikuwa na wakati mgumu kutolewa kwa taarifa hizo.

"Lilikuwa ni jambo la kushangaza, mpaka jana nilihisi kuwa ni rafiki wa papa, mtu wa karibu anayemwamini," aliongeza kusema.

**BBC**



Wanafunzi wakikabiliana na polisi wakati wakiandamana mjini Jakarta, nchini Indonesia juzi. **(PICHA: REUTERS)**

# Donald Trump ampata mrithi wa Ginsburg

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, jana alitarajiwa kumteua Amy Coney Barrett, kuwa kuziba nafasi ya jaji wa mahakama ya juu ya nchi hiyo.

Uteuzi huo ambao unapingwa na wafuasi wa chama cha Democratic, ukithibitishwa Barrett, atakuwa jaji mwenye misimamo mikali kuingia katika chombo hicho cha mwisho kisheria.

Nafasi hiyo, ilikuwa wazi baada ya kifo cha jaji Ruth Bader Ginsburg, ambaye alisifika kuwa na msimamo wa wastani.

Rais Trump, alisema juzi kuwa tayari ameshafanya uamuzi kuhusu chaguo la mrithi wa jaji Ginsburg, huku akijitetea kuwa lilikuwa chaguo zuri. Hata hivyo, alikataa kuweka wazi kutaja jina la mteule wake.

**DW**

## UN wazilaumu Urusi, China kuzuia ripoti

**NEWYORK, Marekani**

WANADIPLOMASIA wa Umoja wa Mataifa, wamesema nchi za Urusi na China, zimezuia kutolewa ripoti inayohusu mgogoro wa Libya.

Wajumbe hao walisema ndani ya ripoti hiyo, kuna sehemu inalaumiwa Urusi na washirika wengine wa kimataifa kukiuka vikwazo vya silaha vilivyowekwa na Umoja wa Mataifa.

Naibu balozi wa Ujerumani katika Umoja wa Mataifa, Gunter Sautter, alisema aliwasilisha suala hilo katika Baraza la Usalama baada ya nchi hizo mbili kuzuia kutolewa kwa ripoti ya kamati inayofuatilia vikwazo dhidi ya Libya, inayoongozwa na Ujerumani.

Ripoti hiyo ambayo shirika la habari la The Associated Press imeiona mapema mwezi huu, ilisema vikwazo hivyo vilikuwa vikikiukwa na serikali ya Libya inayotambuliwa na Umoja wa Mataifa, Uturuki na Qatar.

Pia ilieleza watu wengine waliokiuka ni vikosi vya upinzani vilivyo katika eneo la Mashariki ya nchi hiyo, chini ya kamanda Khalifa Hafter. Vikosi hivyo vinaungwa mkono na Muungano wa Falme za Kiarabu, Urusi na Jordan.

**DW**

## Waziri mkuu Togo ajiuzulu

**LOME, Togo**

WAZIRI Mkuu wa Togo, Komi Selom Klassou, na serikali yake wamejiuzulu.

Taarifa ya Rais wa nchi hiyo, Faure Gnassingbe, alieleza kumpongeza Klassou na mawaziri wake, kufanya kazi kwa juhudi kukuza uchumi, siasa na jamii.

Alitaja hatua hiyo ni ya kutia moyo, licha ya janga la corona kuikumba nchi hiyo na dunia nzima.

Togo ilikuwa ifanye mabadiliko ya kisiasa, lakini mabadiliko hayo yalicheleweshwa kutokana na janga la virusi vya corona. Ushindi wa Rais Gnassingbe, alioupata katika uchaguzi wa mwaka huu, ulikuja baada ya kufanyika mabadiliko ya katiba ambayo ilimruhusu

SAFU

## MAKALA

# Rasilimali za taifa zitunifaishe wote



Na Magabilo Masambu

ZIKIWA zimesalia takribani siku 31 kabla ya siku ya uchaguzi mkuu ambao unatarajiwa kufanyika Oktoba 28, 2020, kati ya mambo muhimu ambayo Watanzania nafikiri tunataka kusikia ni juu ya utajiri wetu wa asili utatumikaje ili kila mwananchi aweze kunufaika bila kujali kwamba ana kazi ya kuajiriwa au kazi zake binafsi.

Azimio la Arusha lenye misingi ya utu linatamka waziwazi juu ya umiliki wa utajiri wa asili linasema "Kwamba raia wote kwa pamoja wanamiliki utajiri wa asili wa nchi, ukiwa kama dhamana kwa vizazi vyao (Nyerere, J.K 1967 Azimio la Arusha uk 2)

Bila kujali imani na itikadi zetu, maandiko yanatabainisha bayana juu ya nini Mwenyezi Mungu alitukabidhi baada ya kutuumba, utajiri huu ulikabidhiwa kwa kila mwana wa nchi, lakini kazi ya kuusimamia na mgawanyo wake unatutegemea sisi wanadamu kupitia kwa viongozi tunaowachagua ili kila mmoja aweze kunufaika nao vizazi mpaka vizazi. Tukitazama historia ya nchi yetu inaonesha kwamba Watanzania walipambana kwa pamoja kuhakikisha kwamba tunajitawala na kuhakikisha kwamba mali na utajiri wetu kama nchi tunaumiliki kwa pamoja, na manufaa yake yanakuwa kwa wote bila kujali kwamba tutakuwa na kazi za kuajiriwa ama kazi zetu binafsi.

Eneo moja ambalo naona haliko sawa linahitaji marekebisho na tunahitaji kulisikia kutoka kwa wagombea wetu sasa ni juu ya pesheni za wafanyakazi, kwamba mfanyakazi wa umma anapofanya kazi baada ya miaka 30 au miaka mitano kwa wabunge hupewa kitu kinaitwa kiinua mgongo, vipi kuhusu wananchi wasiokuwa kwenye ajira rasmi, wao kiinua mgongo chao ni kipi? Kwasababu kama ni ujenzi wa taifa hili tunashiriki pamoja kwa namna mbalimbali, kwa maana kwamba wafanyakazi wanatoa huduma, lakini malipo ya mishahara yao yanatokana na kodi za Watanzania wote wenye kazi za kuajiriwa na wasio na kazi za kuajiriwa kwa maana hiyo hata wale wasiokuwa wafanyakazi wa umma wanashiriki kujenga taifa lao.

Ningefurahi kusikia kutoka kwa wagombea wetu juu ya pensheni za wazee wote (mafao) kwamba Mtanzania yeyote aliyelitumikia taifa hili na kulinda rasilimali za taifa hili anapokuwa mzee basi apate kiinua mgongo anapozeeka bila kujali aliajiriwa ama la!, siwezi kupuuza hizo zinazoitwa huduma za afya za wazee, lakini mbona hata wafanyakazi wa umma huzipata wakiwa kazini na hata wakitoka, lakini nafikiri kama taifa tunahitaji kufikiri upya juu ya namna bora ya kuwapatia pensheni wazee wetu wote nchi nzima bila kujali kwamba ni wafanyakazi wa umma au si wafanyakazi wa umma. Faida kubwa ya kuweka pensheni kwa wazee wote itasaidia kuwafanya Watanzania wote kuwa wazalendo dhidi ya rasilimali asilia kwasababu jambo hilo litawafanya wasiwe sehemu ya hujuma kwasababu watatambua manufaa ya utajiri huwo baadae wanapozeeka, na ikiwa zitafanyika hujuma itakuwa ni sawa na mtu kukata mti alioukalia.

Tumesikia kelele nyingi sana juu ya uzalendo, lakini ukweli ni kwamba uzalendo hauji tu kwa kuuimba au kuupigia mbiu kwamba tuwe wazalendo halafu watu wakawa wazalendo hapana, ili mtu awe mzalendo na kujituma juu ya jambo fulani lazima awe anatambua manufaa ya jambo hilo kwenye maisha yake binafsi.

Wapo wanaosema kwamba uzalendo ni kutenda jambo lenye faida kwa wengine tu na lisikunufaishe binafsi lakini tunasahau kwamba kila mwanadamu ameumbiwa ndani mwake roho ya unafsi yaani ubinafsi wa kujipenda kwanza yeye ndipo afikirie mwingine.

Jambo lolote lisipokuwa lenye manufaa kwa wote hugeuka kuwa ni unyonyaji,wale wanaowaambia kuweni wazalendo ukiyachunguza maisha yao hayafanani na maneno yao maana yake ni kwamba kuna unyonyaji ndani yake, tunataka tuwe na taifa angalau lenye usawa hata kama usawa huo hautakuwa mia kwa mia, lakini baadhi ya mambo tunufaike nayo sote. Katiba yetu bado inatamka kwamba nchi hii ni ya ujamaa na kujitegemea, lakini matendo yetu yanakinzana na ukweli huo, kwasababu ukishatoa huduma zinazotofautiana kwa kiasi kikubwa huwezi kuita tena kama ni ujamaa na kujitegemea, ndiyo maana nashauri kwamba wagombea wetu angalau watueleze vipi hatima ya wazee wasio na kazi zenye ujira, lakini wamekuwa na mchango mkubwa sana katika taifa hili.

Rasilimali na utajiri tulionao leo ni matokeo ya babu na bibi zetu kuamua kututunzia kama ambavyo Mwl. J.K Nyerere amewahi kunukuliwa akisema kwamba madini yaachwe mpaka Watanzania watakapokuwa na akili ya kuyachimba basi wafanye hivyo.

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Filamu ya 'Andha Kanoon' ilivyoliza watu



Na Adam Fungamwango

HE Andha Kanoon he, he Andha Kanoon he, he Andhaaa... Kanoon heee... Ni kipande cha wimbo wa bonge la filamu ya Kihindi, iliyopendwa na watu wengi wa rika mbalimbali kuanzia miaka ya 1980 hadi katikati ya miaka ya 1990.

'Andha Kanoon' ni filamu ambayo ilikuwa haichoshi kuiangalia kutokana na si aina ya uigizaji tu, bali hata maudhui ya filamu yenyewe ambayo kwa kiasi kikubwa yalihuzunisha, kushangaza na kusitikisha kwa wakati mmoja, kiasi cha kusababisha watazamaji wengi kuangua vilio.

Hii ndiyo filamu iliyoongoza kuliza watu kwenye kumbi za sinema na hata wakati televisheni zilivyoanza kuingia nchini na watu kuwa nazo nyumbani.

Ni filamu ambayo pamoja na wengi kutojua kinachozungumzwa, mtiririko wa kile kilichoonekana kilisababisha kinamama, kinadada, watoto na wakati mwingine hata baadhi ya wanaume kuangua vilio. Ilikuwa aghalabu sana kuangalia filamu hiyo halafu ikamalizika hakuna mtu au watu waliotokwa machozi.

Hata leo hii, yeyote yule akiuliza kwenye mitandao ya kijamii ni filamu gani iliyokuwa inaongoza kuliza watu wengi, basi watajibu 'Andha Kanoon', kwa lugha ya Kihindi, iliyokuwa ina maana kwa kiswahili kuwa ni 'Sheria Kipofu.'

Na hata ukiuliza kama kuna mtu aliwahi kulia wakati anaangalia picha hiyo, unaweza kupata watu wengi zaidi watakaosema kuwa waliangua vilio. Na wengine wanaweza kujibu kuwa hata leo wakiiangalia, wanatokwa machozi.

Filamu hii iliingia sokoni rasmi mwaka 1983, vijana wa sasa wanasema ndiyo mwaka iliyoachiwa. Vituko vya filamu hii ni kwamba wakati iko katikati, tayari unasikia kuna watu wenye mioyo midogo wanaangua vilio. Iwe kwenye kumbi au sebuleni.

Wengine wanatoka, hawataki kabisa kuona kinachoendelea kwenye filamu hiyo. Ni filamu iliyojaa taharuki kwa asilimia nyingi sana, kwani kila inapozidi kwenda mbele, ndipo hali kwa wale waliokuwa wanaoonekana kwenye haki inakuwa ngumu.

Kuna watu hadi leo wanasema kuwa ndiyo filamu bora ya Kihindi kuwahi kutokea na haichoshi kuangalia hata leo hii. Miaka ya 1990, ilipokuja teknolojia ya kutafsiri kwa kiswahili, ndiyo kabisa walizidi kuipaisha filamu hiyo.

Tangu miaka ya 1970, 1980 na 1990, kulikuwa na filamu nyingi za Kizungu, Kichina na Kijapani ambazo zilikuwa za kibabe na zilipendwa sana wa Watanzania kuliko za Kihindi.

Mastaa wengi wakiwemo Bruce Lee, Jim Kelly, Wang Yu, Sonny Chiba na wengineo wengi ndiyo waliopendwa sana.

Ujio wa filamu hii ulibadilisha kabisa mitazamo ya vijana wengi wa Kibongo wakati huo ambao wengi wao walikuwa wakipenda zaidi ubabe, filamu za kibabe na si zenye hisia. Hii ilisababisha sasa filamu zingine za Kihindi zilizokuwa zikiingia kutazamwa na kufuatiliwa na watu wengi.

Na sehemu ambayo wengi walikuwa wakilia zaidi kiasi kwamba hata kama walikuwa wanalia kimya kimya, lakini hapa wanashindwa kuvumilia ni pale binti mdogo alipokuwa akiimba wimbo wa 'Rote Rote', ule wa huzuni. Itakumbukwa kuna ule ambao uliimbwa na mmoja wa mastelingi ya picha hilo, Amitabh Bachchan, na ule ambao ameuimba binti yake Amita kwenye filamu hiyo.

Sasa ule wa binti ndiyo ulikuwa ikiwafanya watu, hasa wanawake kulia kwa sauti na wakati wengine kuondoka kabisa, hawataki kuangalia, mpaka labda baadaye, wengine wakakataa kabisa kuangalia. Kipande hicho kinaimbwa 'rote rote, hsana sikho, hasate hasate, rona.' Kilichokuwa kikiwaliza siyo kwamba wanalikuwa wanajua kinachozungumzwa, la hasha. Ni kwamba kipande hicho cha wimbo, Amita awali alikuwa akimwimbia binti yake nyumbani alipokuwa akilia, kwa ajili ya kumbembeleza.

Baadaye Amita alikamatwa na kufungwa. Binti yake mdogo mwenye umri usiozidi miaka mitano hivi akiongozana na mama yake kumtembelea baba yake jela.

Amita alipoiona familia yake, hisia ikampeleka mbali sana, akatokwa na machozi. Binti alikumbuka kuwa baba yake kila akilia nyumbani huwa anamuimbia wimbo huo.

Naye akaanza kuimba wimbo huo kwa ajili ya kumbembeleza baba yake. Wote, baba, mke na binti wakaanza kulia. Ni eneo linalotia simanzi, huzuni na huruma, kiasi kwamba hapo wengi wanashindwa kuvumilia.

Kibaya zaidi ni kwamba huyo Amita mwenyewe amefungwa kwa uonevu tu. Ni askari polisi mwaminifu wa nchi yake, lakini wakubwa zake wala rushwa, wameshirikiana na baadhi ya matajiri wasiotaka kufuata sheria, wakamtafutia kesi ya mauaji.

Alikataa rushwa kwa matajiri, lakini wakubwa zake wapokea rushwa na wakashirikiana na matajiri hao hao kumkamdamiza.

Ni filamu iliyojaa uonevu kwa watu wasafi, wenye mioyo safi na nchi yao na wenye haki, kutoka kwa watu waliopewa dhamana ya kusimamia sheria na haki, kama vile wakubwa wa vitengo, pamoja na baadhi ya mahakimu na majaji ambao ni wala rushwa.

Amita alifungwa jela miaka 30 kwa kuua. Hiyo ilisababisha mkewe na binti yule baadaye wote kufariki dunia. Alipotoka alimuona yule jamaa aliyeambiwa amemuua yupo hai.

Jamaa naye alitimua mbio na kuingia kwenye mahakama ile ile iliyohukumu kesi yake Amitah, hakimu akiwa ni yule yule. Amita aliwauliza kama akimuua anaweza kuhukumiwa tena? Si alikaa miaka 30 jela kwa kudaiwa kumuua mtu ambaye kumbe yuko hai? Na hata akimuua, yeye atarejeshewa mke na watoto wake ambao wamekufa kwa kukosa matunzo bora kutokana na kuwepo jela miaka yote hiyo?

Visa hivyo ni vingine vingi, ndivyo viliifanya filamu hiyo kuwa maarufu na kupendwa sana, waigizaji wake mbali na Amitha ni Rajinikanth, Hema Malini, Danny Denzongpa, Amrish Puri maarufu kama 'mzee Ashanti', Prem Chopra na wengine.

Hii ndiyo filamu ya 'Andha Kanoon' iliyopendwa na wengi waliokuwa wakipenda mno kuitazama, ila kabla ya kuitazama kila mmoja anakuwa na furaha, lakini ikimalizika, kuna wanaolia, walionuna, waliokasirika, waliowaza na wanaotafakari pia.

Hadi leo hii waliowahi kutazama filamu za Kihindi kuanzia miaka ya mwanzoni mwa miaka ya '80 mwishoni mwa '90, watakwambia kuwa hii ndiyo moja ya picha bora waliozowahi kuzitazama na haitokosekana kwenye 10 bora, tano bora, na wala tatu bora.

Zilikuwepo baadhi zenye visa vya kusikitisha kama 'Hatya', 'Disco Dancer', 'Tarzan', lakini filamu hii ilitikisa vilivyo.


**HADITHI**

# HADITHI

WASWAHILI wanasema mshika mawili moja humponyoka, na karamu mbili zilimshinda fisi. Sesilia, msichana mwenye kila sifa ya kuitwa mrembo, anaangukia kwenye mapenzi ya vijana wawili. Mmoja ni fukara na mwingine mwenye uwezo. Kutokana na msichana huyo kutokuwa na msimamo wenye kueleweka, anawaingiza vijana hao kwenye chuki na visasi, vilivyoambatana na wivu uliopindukia kiasi cha kusababisha maafa makubwa. Ni kisa cha kusikitisha, kutisha na kuhuzunisha, lakini kitakachokupa elimu kubwa ya mapenzi.

# Adui Namba Moja- 1

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**



BWANA wee, ondoka na vichungwa vyako, kwani umesikia mama yangu ana upungufu wa damu?"

"Hapana Cecilia, mimi nimekuja kumuona mama tu. Haya machungwa si muhimu sana kwake, najua umeleta chakula, atakula matunda tu akimaliza kula."

"Sasa umesikia sisi hatuwezi kumnunulia machungwa? Yaani umetoka huko na vichungwa vyako vya mia mia, vitano sijui, uje kumletea mama yangu uonekane wa maana sana eee?"

Mashaka alimtazama Cecilia kwa mshangao. Hakuamini maneno hayo kama yanatoka kinywani kwa mwanamke anayempenda. Na yeye mwenyewe alionekana kumpenda, lakini kwa siku za karibuni amebadilika kama kinyonga.

"Sesilia ni wewe kweli?"

"Ndiyo mimi, nitazame vizuri, kwani nimebadilika? Nimebadilika rangi au sura?"

Hata uangaliaji wa Cecilia kwa jinsi alivyokuwa akimtazama Mashaka, ilionekana kabisa kuwa ni dharau.

Alitazama akiwa amemsimamia upande, amemshikia kiuno, halafu macho yakiwa yanamtazama kwa dharau, wenyewe watoto wa mjini wanasema 'kumnyali'.

Alimtazama kuanzia juu na kumshuka hadi chini.

"Sitaki uingie hospitalini kwenda kumuona mama yangu, hakuhusu jicho wala sikio. Siyo mama yako, siyo shangazi yako, wala mkweo, umenisikia?" Cecilia alizidi kumchimba mkwara Mashaka.

Mashaka hakujua la kufanya. Alibaki amesimama na kifuko chake cha machungwa.

Ilikuwa majira saa 10:00 jioni nje kidogo ya geti la kuu la kuingilia la Hospitali ya Mwananyamala jijini Dar es Salaam.

Si watu wengi walioona mzozo huo kutokana na wengi wao walikuwa kwenye pilikapilika ya kuwahi kuona wagonjwa, wengine wakitoka na kuwahi nyumbani. Ni watu wachache tu waliobahatika kuona kilichotokea kati ya Mashaka na Cecilia.

"Ndiyo nishasema hivyo, sitaki kuona ukitia pua yako pale, labda kama una mgonjwa mwingine sawa lakini siyo mama yangu mimi. Upo nyonyo?"

Maneno mazito, ya karaha na ya kukatisha tamaa, yalimvunja nguvu Mashaka na kuhisi mwili mzima kufa ganzi.

Alitamani ardhi ipasuke immeze ili kuondokana na aibu ile anayoipata, tena ikiletwa na mtu ambaye alimtegemea kumpa amani na faraja ya roho lakini leo imekuwa kinyume chake.

**"Sitaki uingie hospitalini kwenda kumuona mama yangu, hakuhusu jicho wala sikio. Siyo mama yako, siyo shangazi yako, wala mkweo, umenisikia?" Cecilia alizidi kumchimba mkwara Mashaka. Mashaka hakujua la kufanya. Alibaki amesimama na kifuko chake cha machungwa. Ilikuwa majira saa 10:00 jioni nje kidogo ya geti la kuu la kuingilia la Hospitali ya Mwananyamala jijini Dar es Salaam.§ §**

Kama maneno yale yangetolewa na mtu mwingine wala asingejali. Lakini na mtu aliyempenda na kujitolea kwa moyo wake wote, ilimuuma na kumkatisha tamaa.

Alitamani kulia, lakini mwili wale na akili havikuwa na ushirikiano wa kufanya vile alivyotaka. Akabaki amesimama.

"Dada vipi, mbona mnagombana na shemeji kuna nini?" Ni sauti mpya iliyosikika kwenye masikio ya Mashaka na Cecilia. Wote waligeuka na kumtazama.

"We Badaka, kuwa na heshima. Mimi dada yako ee, nani shemeji yako? Huyu kinyago?"

"He makubwa, kwani kuna nini?" Badaka aliuliza.

Hakujibiwa.

Badala yake Cecilia alianza kuvuta hatua na kuingia kwenye geti kuu la hospitali. Badaka alionekana kushangazwa na hali ile. Akasimama mbele ya Mashaka.

"We shemeji, kwani kuna nini umemfanya nini dada yangu?"

Mashaka alishusha pumzi ndefu, kiasi cha kumfanya Badaka amuonee huruma.

"Unasikia shemeji, mimi jana ulinitumia meseji kuwa mama anaumwa, baadaye ukanitumia kuwa mama amelazwa, leo jioni ndiyo nimekuja kumtazama, kwa bahati nafika karibu na geti nakutana na Cecy, ndiyo kaanza kunipakia maneno hapa, yaani hukuwapo, lakini malaika wako alikuwapo. Kusema kweli amenikwaza sana. Na amenipiga marufuku kwenda kumuona mgonjwa."

Badaka alimtazama shemeji yake kwa makini akamuuliza "Kwani kuna ugomvi wowote uulitokea baina yenu?"

"Hapana, hakuna ugomvi. Ila dada yako kwa muda wa miezi hii miwili anaonekana amebadilika sana, yaani siyo yule ninayemfahamu mimi. Amekuwa akinijibu maneno ya mkatomkato, nikisema hili yeye anajibu vile." Mashaka alisema huku akikwepesha macho yake yasiangaliane na shemeji yake ambaye alikuwa akimtazama kwa huruma.

"Wewe hujamfanya kitu chochote?"

"Nimfanye nini dada yako mimi?"

"Lo, asilete zake za kuleta hapa, hebu twende, yaani ndiyo anakuzuia kwenda tu kumwona mgonjwa. Hata kama mna ugomvi, mgonjwa anahusika na nini." Badaka alichukua jukumu la kumchukua Mashaka na kwenda naye moja kwa moja kwenye wodi ya wanawake kwenye Hospitali ya Mwananyamala.

Mgonjwa aliyelazwa kitanda namba sita aliitwa Magdalena Rupia. Ndiye mama mzazi wa Cecilia.

Alibahatika kupata watoto watano, watatu wa kiume na wawili wa kike. Cecilia alikuwa wa nne na wa mwisho alikuwa Badaka.

Kutokana na wingi wa watu waliokuja kumwona, wengine ndugu, majirani, rafiki wa ndugu, rafiki wa wafanyakazi wa familia ya mama Cecy, wengi walikuwa hawajuani.

Ni ndugu tu na familia ya mama huyo ndio waliojuana. Walijikuta tu wako pamoja kila mmoja akitaka kumuona mama huyo kwa kumfahamu, au kuvutwa na mtu wa familia yake.

Hilo lilimfanya hata Mashaka asionekane kuwa mtu wa ajabu mbele ya wengine. Tena kizuri zaidi ni kwamba alifika akiwa ameongozana na Badaka, binti wa mwisho wa mama huyo ambaye mumewe alifariki dunia miaka mitatu iliyopita.

Hata hospitali umbea upo vile vile. Wengine walionekana wakinong'onezana. Wakidhani kuwa ni mpenzi wake Badaka. Ni watu watatu tu ndio waliojua nini kinaendelea. Cecy, Mashaka na Badaka.

Baada ya kuongea na mama yake akimjulia hali kwa muda wa dakika tano hivi, alimwita Mashaka aliyekuwa pembeni kidogo.

"Njoo umsalimie mama." Badaka alimwita Mashaka.

Alimsalimia na kumpa pole, lakini pia akimkabidhi kifuko cha machungwa.

"Ahsante mwanangu, nitakula nikishamaliza kula chakula." Mgonjwa alimshukuru.

Mgonjwa hakutaka kumfahamu sana kila mtu anayefika kumtazama kwani wengine aliwafahamu na wengine hakuwafahamu, lakini alifahamu fika kuwa kila mmoja alikuja kwa sababu yake.

Hata ambao hawafahamu walifika kutokana na urafiki na ukaribu wa ndugu na familia yake.

Wakati huo wote Cecy alikuwepo. Yote aliyokuwa yakitokea alionekana kununa na kutazama jicho pembe mdogo wake na Mashaka pia.

Hawakuonekana kujali. Wao waliona mgonjwa ni muhimu zaidi kuliko hayo mengine.

**INAENDELEA JUMAPILI**

## HABARI BURUDANI



## HURUMA YA HAKIMU
# Amber Rutty, mumuwe wanusurika miaka 30

HATIMAYE mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imemhukumu msanii Rutyfiya Abubakary maarufu kama 'Amber Rutty', mumewe Said Bakary na James Charles au 'James Delicious' kulipa faini ya Mil. 11 au kwenda jela miaka 5.

Hukumu hiyo imetolewa baada ya kutiwa hatiani kwa makosa manne ikiwemo kufanya mapenzi kinyume na maumbile.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Godfrey Isaya baada ya mahakama hiyo kujiridhisha pasi na kuacha ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

"Nimezingatia hoja za pande zote mbili na athari za makosa haya, ni kweli washitakiwa wote vijana na wanategemewa, nimeona mshitakiwa wa kwanza anajutia, kutokana na mazingira ya kesi hii adhabu yake ni miaka 30 kila kosa ambapo nikiwafunga mtapotea kabisa" amesema Hakimu Isaya.

"Hivyo kwa mazingira mliyoyasema na lengo la adhabu ni kujirudi, mshitakiwa wa kwanza (Amber Rutty) utalipa Milioni 3 ama jela miaka 5, mshitakiwa wa pili, Saidi Bakari, utalipa faini ya milioni tatu ama jela miaka 5 na mshitakiwa wa tatu James Charles atalipa faini milioni tano ama jela miaka mitano na adhabu zitaenda sambamba" ameongeza.

Mpaka jana washtakiwa wote walikuwa mahabusu hadi hapo watakapolipa faini hizo.



# CHIDI BENZ
## KUANDAA FILAMU YAKE

KAMA unataka kujua raha na machungu aliyopitia Rapa, Chidi Benz, basi kaa tayari kwani yupo mbioni kuandaa filamu inayoelezea safari ya maisha yake.

Akizungumza katika kipindi cha Friday Night Live, kinachorushwa na E ATV, Benz, amesema wazo hilo limetokana na mpenzi wake, ambaye alimshauri kuachia filamu hiyo ili Watanzania wajifunze kupitia kwake.

"Jana mpenzi wangu ameniambia hivyo na tulikuwa tunajadiliana kuhusu hilo, akaniambia nikifanya filamu yangu itakuwa poa sana ila inatakiwa kupangwa vizuri ila sio kukurupuka maana itakuwa kama bangi". amesema.


# BARAKA HATA WENZAKO WANAKATAA

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Baraka The Prince, amesema kuna baadhi ya wasanii wanajihusisha na mambo ya kishirikina katika muziki wao kama njia moja ya kupata mafanikio.

Akizungumza na EATV, Baraka amesema kwa upande wake hana imani hiyo, yeye huwa anamuamini Mungu kama mganga wake mkuu katika muziki.

"Siamini sana mambo ya ushirikina na sijawahi kufanya, ila nasikia tu watu wanasema, mimi nimeweza kufanikiwa bila kwenda kwa waganga, mimi mganga wangu mkuu ni Mungu, mwanadamu mwenzangu atawezaje kunifungulia mambo, naamini sana katika sala na Mungu" amesema Baraka The Prince





# ARTETA:
## ARSENAL BADO IPO SOKONI

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amesema Arsenal imejianda kwa namna yoyote kama kutatokea nafasi ya kusajili kabla ya pazia la dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto kufungwa Oktoba 5, mwaka huu.

Kuelekea mechi zake mbili dhidi ya Liverpool wiki hii, 'Washikabunduki' hao wamekuwa wakihusishwa na nyota wa Atletico Madrid, Thomas Partey, kiungo wa Chelsea, Jorginho na nyota wa Lyon, Houssem Aouar.

Lucas Torreira amekuwa akihusishwa na Atletico katika dili ambalo linaweza kuongeza nafasi ya Arsenal kumpata Partey.

Wakati Arteta hakuwa na taarifa yoyote kuhusu usajili mpya kabla ya kuivaa Liverpool kwenye Ligi Kuu kesho Jumatatu, amebainisha kuna nafasi ya kufanya usajili.

"Bado tumefungua milango ya kuimarisha timu yetu," alisema kuelekea mchezo huo utakaopigwa kule kwenye dimba la Anfield.

"Tunaangalia machaguo tofauti, ikitemgemea na nini kitatokea kwa baadhi ya wachezaji wetu hapa. Tumeshajiandaa kama kutatokea lolote.

"Hatuna kipya juu ya Lucas au mchezaji mwingine yeyote kwa wakati huu na samahani siwezi kuwazungumzia wachezaji wanaocheza klabu nyingine."

## BARCA BADO INA KIKOSI CHA USHINDANI- ZIDANE

**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane anaamini Barcelona wana kikosi chenye uwezo wa "kupambania kila kitu".

Baada ya kumaliza msimu wa 2019-20 bila taji lolote Ronald Koeman anakijenga upya kikosi hicho cha Blaugrana, ambacho kimewaachia wachezaji wake kama Luis Suarez, Arturo Vidal, Ivan Rakitic, Arthur na Nelson Semedo kuondoka.

Philippe Coutinho amerudi kutoka alikokuwa akicheza kwa



mkopo kule Bayern Munich na Miralem Pjanic amejiunga nao kutoka Juventus, huku Lionel Messi akiamua kubaki baada ya awali kuomba kuondoka.

Zidane, ambaye jana Jumamosi kikosi chake cha Madrid kiliwafuata Real Betis, amesema Barca wana kikosi imara cha kutoa changamoto ya mataji msimu huu.

"Tunawaheshimu. Licha ya kujua kile kinachoendelea kwao naamini kwamba bado wana kikosi imara sana," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nafikiri klabu ina mambo yake na magumu yao. Nafikiri Barcelona, katika suala la timu na kikosi, ni klabu ambayo itapigania kila kitu.

"Sina shaka kwa hili."

## JESUS AIPA PIGO MANCHESTER CITY

**MANCHESTER, England**

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Gabriel Jesus, anatarajiwa kuwa nje ya dimba angalau hadi katikati ya mwezi ujao baada ya kuondolewa katika kikosi cha Brazil kitakachoivaa Bolivia na Peru kwenye michuano ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia mwaka 2022.

Majeraha ya Jesus hayajawekwa wazi, licha ya Shirikisho la Soka la Brazil (CBF), kuthibitisha kwenye taarifa yake kwamba City imewaarifu nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, hatajiunga nao.

"Timu yake ya Uingereza iliwasiliana na daktari wa timu ya Taifa ya Brazil, Rodrigo Lasmar, na kuripoti majeraha ya mchezaji huyo baada ya mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Wolves Jumatatu," ilisema taarifa hiyo.

Straika wa Hertha Berlin, Matheus Cunha ameongezwa kwenye kikosi hicho cha kocha, Tite, akiitwa kwa mara ya kwanza katika timu ya taifa ya wakubwa baada ya kuifungia Brazil chini ya umri wa miaka 23 kwenye mashindano ya Mataifa ya CONMEBOL mapema mwaka huu.

Jesus alifunga bao la mwisho kwenye ushindi wa 3-1 pale katika dimba la Molineux na alionekana kuendelea kuwa chaguo la kwanza la kocha, Pep Guardiola, hasa kwa kuwa Sergio Aguero anaendelea kujiuguza baada ya kufanyiwa operesheni.

Sasa Man City haitakuwa na mshambuliaji wake huyo muhimu kwenye mchezo wa leo Jumapili wa Ligi Kuu dhidi ya Leicester City.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SUAREZ: SABABU MESSI KUNILILIA BARCA HII HAPA

●●●Ananijua vizuri na anajua uwezo wangu na kujiamini kwangu, ni ishara nzuri na fahari kuondoka huku...

**MADRID, Hispania**

LUIS Suarez amesema ajisikia fahari kwa kutetewa na Lionel Messi baada ya uhamisho wake wa kwenda Atletico Madrid kutoka Barcelona.

Suarez mwenye umri wa miaka 33, alijiunga na Atletico kwa euro milioni sita wiki hii akitokea pale Camp Nou.

Rafiki yake wa karibu na nyota wa Barcelona, Messi aliwashushia lawama miamba hao wa Catalunya Ijumaa, akisema Suarez "alifukuzwa" na "hakuna cha zaidi kilichomshangaza" yeye.

Suarez, ambaye alishinda mataji 13 akiwa na Barca, alisema alijisikia fahari kuondoka huku kukiwa na mtazamo chanya namna ile kutoka kwa wachezaji wenzake.

"Leo ananijua mimi vizuri na anajua uwezo wangu na kujiamini kwangu. Ni ishara nzuri na fahari kuondoka huku kukiwa na mtazamo chanya nyuma yangu," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Sasa nimeondoka na kujiunga na kikosi hiki cha ushindani na chenye hamasa kubwa."

Suarez alifunga mabao 21 kwenye mechi 36 msimu uliopita, lakini sasa kocha mpya wa Barca, Ronald Koeman amebainisha hakuna nafasi kwa nyota huyo wa Uruguay wakati akikijenga upya kikosi hicho cha Blaugrana.

Mshambuliaji huyo kujiunga na klabu nyingine kubwa nchini Hispania ilikuwa hamasa kubwa kwa upande wake.

"Hamasa kubwa kwangu kwa kuja kwenye klabu kubwa nchini Hispania, Atleti," alisema Suarez.

"Ina wachezaji wakubwa, wenye ushindani mkubwa ambao mara zote wanapambana kuwania nafasi ya juu katika ligi.

"Mashabiki na kocha (Diego Simeone) pia wamenihamasisha sana."

Atletico itaanza msimu wa 2020-21 kwa kucheza nyumbani dhidi ya Granada leo Jumapili kwenye mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu ya Hispania.

## KWA UFUPI

**LAMPARD AMTAKA RICE**

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, ameitaka klabu hiyo ya Stamford Bridge kujaribu kumsajili kiungo wa West Ham, Declan Rice mwenye umri wa miaka 21. Kama nyota huyo wa kimataifa wa England akitua hapo kuna nafasi kubwa kwa kiungo wa Italia, Jorginho kuhamia Arsenal. ***(Mirror)***

**PSG YAJITOSA KWA RUDIGER**

PARIS St-Germain inawania kumsajili mlinzi wa Chelsea, Antonio Rudiger, lakini wanasubiri kuona kama nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 27, atapatikana kwa mkopo au usajili wa kudumu. (Telegraph)

**SPURS YAMNYATIA SKRINIAR**

TOTTENHAM Hotspur ipo kwenye mazungumza ya kumsajili mlinzi wa kimataifa wa Slovakia, Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 25 lakini hawatakuwa tayari kukubali kulazimishwa kulipa ada inayotakiwa na Inter Milan ya pauni milioni 55. ***(Sun)***

**INTER KUMSAJILI SMALLING**

INTER Milan watajitosa kumsajili mlinzi wa Manchester United na England, Chris Smalling mwenye umri wa miaka 30, kama watamuuza Skriniar kwa Tottenham Hotspur. ***(Football Italia)***

**KANTE KWENYE RADA ZA INTER**

KLABU ya Inter Milan pia inaangalia uwezekano wa kumsajili kiungo wa Chelsea, N'Golo Kante ili nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, akaungane na kocha wake wa zamani pale Blues, Antonio Conte. (Gazetto dello Sport via Mail)

**KOUNDE YUPO SOKONI SEVILLA**

KLABU ya Sevilla inatarajia ofa ya pili kutoka Manchester City kwa ajili ya mlinzi wake wa pembeni, Jules Kounde na inawezakana wakashindwa kuikataa ofa ya kuanzia euro milioni 65 hadi 70 kwa ajili ya Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(ESPN)***

**ARSENAL RASMI KWA AOUAR**

ARSENAL imetoa ofa ya pauni milioni 32 ili kumsajili kiungo wa Lyon, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 22, lakini klabu hiyo ya Ligue 1 inataka pauni milioni 54 ili kumuachia kiungo huyo wa kimataifa wa Ufaransa. ***(RMC Sport, via Metro)***

**DEPAY BADO LULU BARCA**

STRAIKA wa Lyon, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 26, anaonekana kuwa chaguo la kwanza la Barcelona ili kuimarisha safu yao ya ushambuliaji. ***(Mundo Deportivo via Mail)***

**STRAIKA LIVER AGOMBEWA**

STRAIKA wa Liverpool na England, Rhian Brewster mwenye umri wa miaka 21, anawaniwa kujiunga na Sheffield United, huku Aston Villa na Brighton pia zikimuwania nyota huyo mwenye umri wa miaka 20. ***(Sheffield Star)***

**LAMPARD KUTETA NA KEPA**

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, anapanga kufanya mazungumzo na golikipa wake, Kepa Arrizabalaga mwenye umri wa miaka 25, baada ya kumsajili kipa wa kimataifa wa Senegal, Edoaurd Mendy, 28. ***(Star)***

**LEEDS YAMUWANIA KOOPMEINERS**

LEEDS United inawania kumsajili kiungo wa Uholanzi, Teun Koopmeiners mwenye umri wa miaka 22, kutoka AZ Alkmaar. ***(Telegraph)***

HABARI MICHEZO

# KAHATA AKUNWA USHINDANI NAMBA KUIIMARISHA SIMBA

Na Mwandishi Wetu

HUKU akikiri kuwa ushindani wa namba ndani ya kikosi cha Simba umeongezeka kutokana na kila nafasi kuwa na wachezaji wenye viwango vya juu, kiungo mnyumbulifu wa timu hiyo, Mkenya Francis Kahata amesema anaifurahia hali hiyo kwani inaifanya timu kuwa bora.

Tangu kuanza kwa msimu huu, kabla ya mechi ya Simba dhidi ya Gwambina FC katika Uwanja wa Mkapa jana, Kahata amecheza mara moja tu tena akitokea benchi, wakati timu hiyo ikivuna pointi saba kwa kushinda michezo miwili na kutoka sare moja.

Lakini Kahata, amemwambia mwandishi wetu kuwa anayafurahia maisha ndani ya kikosi cha Simba na ataendelea kupambana ili kupata nafasi ya kuanza.

"Kila mchezaji anayecheza anacheza kwa ajili ya timu, na timu ikishinda tumeshinda wote, ushindani ni mkubwa lakini hali hiyo ni nzuri kwa wachezaji kwa sababu inakuwa ni changamoto kwa kila mchezaji kuongeza juhudi mazoezini.

"Mwanzoni mwa msimu sikuwa fiti kwani nilipata majeraha ingawa sasa yamepona na nipo fiti kucheza, lakini ushindani wa namba ni mkubwa na hilo ndilo linalotakiwa, sina wasiwasi najua nitacheza tu," alisema Kahata ambaye msimu uliopita alionyesha kiwango cha juu na kuwa kipenzi cha mashabiki wa timu hiyo.

Nafasi ya kiungo anayocheza Kahata, licha ya tangu msimu uliopita kusheheni wachezaji wengi wenye vipaji, lakini klabu hiyo imeongeza viungo wengine akiwamo Bernard Morrison pamoja na Rally Bwalya ambaye anaweza kucheza nafasi zaidi mbili dimbani.

Hata hivyo, Kahata anaamini ni muda tu unahitajika na kuongeza juhudi mazoezini ili kumshawishi Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbelgiji Sven Vandenbroeck kumpanga katika kikosi cha kwanza ambacho mara nyingi amekuwa akimwanzisha Morrison katika nafasi hiyo.

# Kocha Mbeya City sasa kubadili kikosi

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Mbeya City, Amri Said, amesema atalazimika kukibadilisha kikosi chake hasa safu ya ushambuliaji kwa sababu kimekuwa ikikosa mabao mengi kutokana na kutokuwa na utulivu.

Akizungumza baada ya kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Namungo FC, Amri alisema pamoja na kupoteza mechi hiyo, lakini kikosi chake kilipambana na kucheza vizuri, ila tatizo limekuwa ni kuweka mpira ndani ya wavu.

**"Vijana wamecheza vizuri, lakini tatizo tu lilonalo kwa sasa ni kufunga magoli. Nina vijana wadogo ambao nimewaamini, lakini wamekosa utulivu wanapokuwa golini na uzoefu, sasa naangalia uwezekano wa kubadilisha kikosi na hasa kwenye safu ya ushambuliaji," alisema.**

Amri alisema kwenye kikosi alichonacho, anao baadhi ya washambuliaji wazoefu ambao kwenye mechi zinazofuata atawatumia, lakini pia kuna uwezekano hata kipindi cha dirisha dogo la usajili kusaka nyota wazoefu wa ligi ili kuwaongezea nguvu vijana alionao.

Kwenye mechi dhidi ya Namungo, Mbeya City ilionekana kukuruka huku na huko kwa kufanya mashambulizi mfululizo, lakini washambuliaji wake walionekana kukosa mabao ya wazi ambayo kama wangetumia nafasi vizuri, basi ingeweza hata kuondoka na ushindi, achilia mbali kutoka sare.

Ijumaa iliyopita, Mbeya City ilipokea kipigo cha nne mfululizo kutoka kwa Namungo na kuifanya timu hiyo kuendelea kuburuza mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania, ikiwa imeshamaliza raundi ya nne.

Ilianza kwa kuchapwa mabao 4-0 dhidi ya KMC, baadaye 1-0 dhidi ya Yanga, 1-0 dhidi ya Azam FC kabla ya kufungwa bao 1-0 tena dhidi ya Namungo.

Kati ya mechi hizo nne, mbili imefungwa ugenini na mbili nyumbani, lakini ikiwa haijafunga goli lolote mpaka sasa.

KAZI IMEANZA...



Mshambuliaji wa Kagera Sugar, Yussuf Mhilu, akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao pekee wakati ikishinda 1-0 dhidi ya KMC FC, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba juzi. Ushindi huo ni wa kwanza kwa Kagera Sugar tangu imeanza ligi msimu huu. **MPIGAPICHA WETU**

# Kisinda awatuliza mashabiki Yanga

Na Mwandishi Wetu

LICHA ya kiwango alichoanza kukionyesha kupokelewa vizuri na mashabiki wa Yanga, winga wa timu hiyo Mkongomani Tuisila Kisinda amesema anajiona bado hajacheza katika kiwango chake cha juu jambo ambalo anafanya kila liwezekanalo kuhakikisha anarejesha ubora wake na kutoa mchango mkubwa kwa timu kufanya vizuri.

Yanga leo itashuka katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro kuvaana na wenyeji wao, Mtibwa Sugar baada ya kutoka kuvuna pointi tatu dhidi ya Wakatamiwa wa Kagera, Kagera Sugar kwenye dimba la Kaitaba.

Na tangu msimu huu umeanza, Kisinda ambaye amejiunga na Yanga msimu huu akitokea AS Vita ya kwao DR Congo, amekuwa katika kikosi cha kwanza cha Mserbia Zlatko Krmpotic, ambapo wamefanikiwa kushinda mechi mbili na kutoka sare moja.

Lakini, Kisinda amesema bado hajacheza na kufikia katika kiwango chake cha juu jambo ambalo anapambana ili kurejea katika hatua hiyo na kuweza kuisaidia timu yake kwenye mechi za Ligi Kuu zinazoendelea.

"Bado sijarejea katika ubora wangu, mashabiki wanatakiwa kuwa na subira, lakini waendelee kuiunga mkono timu yao, sijacheza katika kiwango kizuri ila naamini kwenye michezo ijayo mambo yatabadilika tu.

Akiizungumzia Ligi Kuu Bara, Kisinda alisema: "Kuna mambo najifunza kupitia ligi hii ambayo nimegundua kuwa inawachezaji wengi wazuri na ina ushindani mkubwa hivyo inahitaji kupambana ili kupata matokeo na mimi nipo tayari kwa hilo."

Hadi sasa Kisindi ametengezeza pasi moja ya bao, akifanya hivyo wakati Yanga ikishinda 1-0 dhidi ya Kagera Sugar baada ya kuambaa na mpira na kuingia nao ndani ya 18 kabla ya kumpasia Mkongomani mwenzake, Tonombe Mukoko aliyefunga bao hilo dakika ya 72 kwenye Uwanja wa Kaitaba.

Hata hivyo, Kocha wa Yanga, Zlatko amesema tatizo kubwa ndani ya kikosi hicho si uwezo wa mchezaji mmoja mmoja, bali timu hiyo haijawa na muunganiko mzuri jambo ambalo pia linachangia kushindwa kufunga mabao mengi.

Zlatko amesema, kitendo cha kutokuwa na muda wa kutosha wa kujiandaa na msimu mpya, ndicho kinachoingharimu timu hiyo licha ya kufanya usajili mzuri, lakini anaamini kadri timu inavyoendelea na mechi za ligi, muunganiko huo utapatikana na kuanza kupata ushindi wa kishindo.

# Michezo

Jumapili Septemba 27, 2020


Nipashe




**Suarez: Sababu Messi kunililia Barca hii hapa**

UKURASA 22

## HUAPATI KITU...




Mshambuliaji wa Manchester United, Anthony Martial akijaribu kufunga lakini kipa wa Brighton, Mat Ryan akionyesha umakini langoni mwake kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa The Amex jana. United ilishinda kwa mabao 3-2. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YATAMANI SUKARI YA MTIBWA

### Zlatko ataka wailambe zaidi leo kuliko ile ya Kagera, Katwila awaonya asema...

**Na Somoe Ng'itu, MOROGORO**

BAADA ya tambo na majigambo ya hapa na pale kutawala zaidi ya wiki moja, hatimaye siku iliyosubiriwa imefika kwa Mtibwa Sugar kuwakaribisha Yanga katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani hapa.

Yanga itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kutoka 'kulamba sukari' ya ndugu zao Mtibwa Sugar, kwa ushindi wa bao 1-0 walioupata ugenini dhidi ya Kagera Sugar huku pia 'Wakata miwa' hao wa Morogoro wao wakiilowesha sukari Ihefu FC ya jijini Mbeya kwa ushindi kama huo.

Lakini pia Yanga itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 na Mtibwa Sugar msimu uliopita katika mechi ya mzunguko wa pili dimbani hapo ikiwa ni baada ya raundi ya kwanza ya ligi hiyo kushinda kwa bao 1-0 katika Uwanja wa Mkapa.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga yenye pointi saba iko katika nafasi ya tano (kabla ya mechi za jana), wakati Mtibwa Sugar yenyewe ilikuwa nafasi ya nane baada ya kujikusanyia pointi tano.

Kocha wa Yanga, Mserbia Zlatko Krmpotic, aliliambia gazeti hili kuwa kikosi chake kiko imara na tayari kwa mchezo huo na wachezaji wake wameimarika tofauti na walivyokuwa wakati msimu huu unaanza.

Zlatko alisema kila mchezaji ameahidi kucheza kwa kiwango cha juu na kutimiza vema majukumu atakayowapa huku akijiandaa kukutana na ushindani kutoka kwa wenyeji Mtibwa Sugar.

Kocha huyo alisema ameyafanyia kazi upungufu wote uliyoonekana katika michezo iliyotangulia na amewakumbusha wachezaji wake kuongeza umakini wanapokaribia eneo la kufunga.

"Kwanza timu inahitaji ushindi, hilo tumefanikiwa, lakini kwetu sasa tunahitaji kupata mabao zaidi ili kujiweka nafasi nzuri, kufunga goli moja haitoshi, tumelizungumza na kulifanyia kazi, matumaini yangu kesho (leo), tutaonekana tofauti," alisema Zlatko.

Aliongeza amewapa mbinu mpya washambuliaji wake ambao wanaongozwa na Michael Sarpong kubadilika na kuwasoma wapinzani wao kabla ya kufanya mashambulizi.

Mshambuliaji Mkongomani, Tuisila Kisinda, alisema kwake hana wasiwasi na Uwanja wa Jamhuri na kueleza viwanja vya Afrika vinafanana.

" Walete Mtibwa, Uwanja kwangu si tatizo, viwanja vya Afrika vinafanana, niko tayari kuisaidia timu yangu kupata matokeo mazuri katika mechi hiyo," Kisinda alisema.

Naye Meneja wa Yanga, Hafidh Saleh, alisema maandalizi ya mechi hiyo yamekamilika na kila mchezaji amekabidhiwa jukumu kwenye eneo lake.

Hafidh alisema kikosi chao kina mchezaji majeruhi mmoja tu ambaye ni Mapinduzi Balama, hivyo waliobakia wana nafasi sawa ya kucheza katika mchezo wa leo.

"Tumetulia na tunaomba Mungu atuamshe salama hapo kesho (leo), muda na saa tutaongea, tunaamini hatutawaangusha mashabiki wetu," alisema meneja huyo.

Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, alisema vijana wake wako imara na wamejipanga kuendeleza kasi ya ushindi waliyoianza kwenye ligi hiyo msimu huu.

Katwila alisema kikosi chake kimeimarika tofauti na walivyokuwa msimu uliopita na amewataka Yanga wasiende na "matokeo mfukoni."

"Nina maingizo mapya katika kikosi changu, ninaamini wataisaidia timu na wameimarika zaidi baada ya kucheza mechi tatu, tutasukuma ngome yao, tunajua mahali imara na kwenye mapungufu, tumejiandaa kufanya makubwa, wanajua tulichowafanya Zanzibar, wasitegemee njia nyepesi," Katwila alisema.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya Ruvu Shooting dhidi ya Biashara United wakati Mwadui FC watawakaribisha Ihefu FC kwenye Uwanja wa Mwadui Complex ulioko mkoani Shinyanga.

# Dube aigandisha Azam FC kileleni

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa na Mzimbabwe Prince Dube dakika moja kabla ya mechi kumalizika, limeifanya timu ya Azam kurejea kileleni ikiiengua KMC ambayo ilikuwa ikiongoza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa raundi tatu mfululizo.

Straika huyo alitumia makosa ya mabeki wa Prisons kuruka na mtu mmoja hewani na kumsahau mchezaji huyo hatari aliyepiga kichwa maridadi mpira wa krosi kutoka winga ya kushoto na kujaa wavuni, huku kipa Jeremiah Kisubi akishindwa hata kutingishika.

Ni mechi ambayo Prisons itabidi ijilaumu yenyewe kwani ilikosa mabao mengi ya wazi, lakini pia ikiibana Azam kwa muda mwingi wa mchezo, kabla ya kosa moja ililofanya dakika za mwisho lililotumiwa vema na wapinzani wao.

Wakati Dube akiipa ushindi Azam wa bao 1-0 dhidi ya Prisons kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga, yeye mwenyewe lilikuwa ni bao lake la tatu kufunga msimu huu kwenye mechi nne tu ambazo amecheza.

Kwa ushindi huo, Azam inafikisha pointi 12 ikishinda mechi zote nne ilizocheza, imefunga mabao matano ikiwa haijaruhusu nyavu zake kutingishwa.

Hakuna timu yoyote inayoweza kuishusha Azam kwenye mechi za raundi ya nne, hivyo itaendelea kuongoza kwa wiki nzima hadi kwenye mechi za raundi ya tano.

Hii ni baada ya timu zilizoshinda mechi tatu mfululizo, Dodoma Jiji na KMC zote kupoteza kwenye mechi za raundi ya nne.

KMC ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba juzi na Dodoma Jiji kukumbana na kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi jana.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >